

NAWE HUI



Asante, Ndugu Neville. Bwana awabariki. Niliingilia jambo fulani, sivyo? Nataka kumshukuru Bwana, sana sana, kwa kumshughulikia mvulana wa Ndugu Capps. Ilitukia tu kwamba huu ndio wakati mfupi ambao mimi hurudi Indiana. Najua ya kwamba wao hawarekodi haya; nafikiri hawayarekodi. Na kwa hiyo basi sioni mtu ye yote pale ndani, kwa hiyo wao... Nimerudi kusudi niende kuwinda kindi. Na kwa hiyo nafikiri itambidi Charlie kunivumilia, yeye na Nellie, na hao huko Kentucky, sasa kwa siku moja ama mbili, kuwinda kindi. Kwa hiyo, afadhali nikose kitu cho chote, namna nyingine yo yote ya maburudiko, halafu nije hapa kwenye... mnamo katikati ya Agosti, kisha niende kuwinda kindi pamoja na Charlie na Banks, na hao wote. Kwa namna fulani ni jambo nililozoea. Na kwa hiyo nilimchukua Joe...

² Wakati tulipokuwa hapa ule wakati mwingine, kila mtu aliagua, badiliko la kwenye ile hali ya hewa yenye joto sana kufikia hii—hii hali ya hewa yenye baridi mliyo nayo hapa. Najua mnafikiri hii si baridi, bali hebu mje huko Arizona wakati mmoja. Ilikuwa mia moja na kumi kwenye kivuli nilipoondoka juzijuzi asubuhi; halafu kwenye usiku wa manane, usiku, wakati hewa yenye baridi inaposhuka kutoka milimani, ilikuwa bado tisini na sita. A-ha. Mnaona, hiyo ni kwenye usiku wa manane, wakati hewa baridi ilipokuwa inashuka. Na kwa hiyo ni... Mahali hapo ni sawa kwenye msimu wa kipupwe, bali ni pa nge na mijusi kwenye msimu wa kiangazi, si binadamu. Hata wanyama wote huondoka wanaenda milimani. Hawawezi kweli kuivumilia.

³ Nami nilikuwa nimetoka na ninalenga shabaha bunduki yangu. Mimi...Kwa namna fulani nataka tu kuwaambia juu ya mvulana mdogo wa Capps. Nami nilisema...Na, Joe, itanibidi tu kumpa bunduki, maana anaweza kunishinda kulenga shabaha. Tulikuwa tumekwisha ilenga shabaha, nami nilikuwa—nilikuwa nikipigilia visiki kwenye yadi hamsini. Nami nikamwambia—nikamwambia Joe...Joe alisema, “Baba, ninaamini ningeweza kufanya hivyo.” Maskini jamaa huyo alikuwa ameumwa na kichwa. Nilikuwa nikimwomba, homa kali. Aliondoka akaenda mahali pa kulenga shabaha pamoja nami, nami...

⁴ Duara yo yote ya mbili juu ya kumi katika bunduki ya ishirini na mbili, inavuka mstari wake wa kulenga shabaha kwenye yadi ishirini na tano; inaingia tena kwenye hamsini, vivyo hivyo tu, kama ilikuwa ya mbili juu ya kumi. Kwa hiyo basi...Nami nilikuwa nimeipiga kwenye yadi ishirini na tano. Na kwa hiyo nilikuwa na visiki vingine viwili nami nilivipigilia,

na kama Joe hakuvipigilia hivyo visiki viwili! Sikuwa na visiki vingine, kwa hiyo nikaweka kipande kidogo cha maskini njiwa wa udongo aliyekuwa amepasuliwa kule, ambao walenga shabaha huwapiga risasi, kama tu robo inchi kutoka upande mmoja mpaka mwingine, nami nikamlenga shabaha kwenye yadi hamsini, naye akamkata nusu katika vipande viwili. Nayo ile darubini ilikuwa imelengwa kwa ajili ya macho yangu, akiwa tu mwenye umri wa miaka mingi kidogo na alivyokuwa. Kwa hiyo akasema, “Unajua nini? Lazima nipitie kwa Billy na kumwambia aondoke kwenye miguu yangu tangu sasa na kuendelea.” Mnaona? [Ndugu Branham pamoja na kusanyiko wanacheka—Mh.]

⁵ Kwa hiyo, kwa hiyo nikasema, “Vema, hebu nikwambie,” kasema, “hebu tushuke twende tukamwonyeshe Ndugu Norman hicho.”

⁶ Nikasema, “Joe, katika mashindano kila mahali ulimwenguni, sijali ingekuwa ni nani, hakuna mtu...” Sasa, vile visiki havikuwa vimeshindiliwa upande, vilikuwa vimeshindiliwa moja kwa moja. Na kipande hicho, hakikuwa kimepita, nafikiri, robo inchi, na chenye kina cha moja juu ya kumi na sita, na urefu wa robo inchi kwenda juu, alikikata nusu katikati vipande viwili, kwenye yadi hamsini. Nikasema, “Hakuna mtu ulimwenguni angaliweza kupiga shabaha nzuri zaidi. Wangaliweza, mabingwa, wangaliweza kufanya jambo lile lile, bali hungaliweza kupiga risasi tatu nzuri zaidi kuliko hizo.” Hivyo visiki, havikupindika, ni shimo laini tu katika ile karatasi ambamo visiki vilipitia. Nami nikasema, “Hakuna mtu angaliweza kupiga shabaha nzu—nzuri zaidi.” Vema. Nafikiri kichwa chake kilipoa papo hapo.

⁷ Nami nikasema, “Vema, hebu twende tukamwonyeshe Ndugu Norman hiki,” ambaye hufanya kazi na *Field and Stream*, duka la vifaa vya michezo la Ndugu Tony Stromei.

⁸ Akasema, “Hebu tupitie kwa Billy kwanza.” Yeye akasema, “Na—nataka tu kumwambia Bubby kitu.” Mnaona? Na, kwa kweli, ndugu yake hajapata kufanya vizuri hivyo. Kwa hiyo akasema, “Tutapitia kule kwanza.”

⁹ Na mara nilipofikia mlangoni, Billy alikuwa bado amevaa pajama. Naye akasema... Tulishuka tukaenda kule mapema, maana kunakuwa na joto sana. Na kwa hiyo akasema... Simu ikalia. Nami nikasema... Yeye kwa namna fulani aliniangalia hivi. Nikasema, “Labda ni simu ya mgonjwa.” Na ilikuwa ni Ndugu Capps kwa ajili ya mvulana wake, akiwa kwenye chumba cha kufanyiwa upasuaji wakati huo, huku mchoto wa kitambi cha tumbo pamoja na huyo vikingoja bado. Na sasa hivi ameniambia mvulana wake anapata nafuu vizuri sana, sana.

¹⁰ Kwa hiyo, mnaona jinsi Mungu alivyolitenda jambo hilo, hata katika sauti ya huyo mvulana mdogo, Joe? Badala ya

kushuka kwenda kwa Ndugu Norman, hangalikuweko, ndipo wakaja. Na mimi na Ndugu Capps tukaungana. Sisemi maombi yetu ndiyo yaliyotenda jambo hilo, bali ilimaanisha kitu fulani kwake kwa sisi kuwasiliana namna hiyo. Na, kwa kweli, hiyo ndiyo... Wakati inapokubidi—huna budi kuwa na imani katika yale unayofanya. Mnaona? Na, hiyo, imani yake kupiga simu, naye Billy alikuwa...

¹¹ Walikuwa wakiweka fedha. Akasema, “Hii haina budi kuwa ni ya kutoka mbali sana,” kasema, “yeye alikuwa akiweka karibu dola tano za fedha taslimu, katika ninino tatu...kwa kupiga simu muda wa dakika tatu.” Nami nikafikiri ingekuwa inatoka New York ama huko nje kwenye moja ya visiwa ama po pote pale. Lakini akapiga simu ya mtu mmoja kwa mwingine, apate kumpata Billy badala ya Loyce, mnaona, na hivyo ndivyo ilivyomgharimu kufanya jambo hilo.

¹² Na sasa mvulana wake anapata nafuu. Ndugu Capps alisema daktari alikuwa amempa matumaini madogo sana ya kupona, mnaona, kutoka kwenye huko kupasuliwa. Nasi tunamshukuru Mungu asubuhi ya leo kwa ajili ya jambo hili, tuna furaha sana kwa jambo hili.

¹³ Naam, tulirudi, kuelekea mapambazuko asubuhi hii, nami nilipata usingizi wa masaa matatu, na—nami nimechoka sana. Lakini wakati kanisa...wakati unawadia wa kuja kanisani, naam, ninashuka ninakuja. Ndipo...

¹⁴ Bwana akipenda, sasa sina budi kushuka kwenda Kentucky, kama nilivyosema. Halafu nikaahidiwa kuzungumza Jumapili moja nilipokuwa nimerudi hapa, na afadhali niifanye Jumapili hii ijayo, kwa sababu inayofuata itakuwa...sina budi kurudi. Kwa sababu ninaondoka tena, kule Canada. Kwa hiyo a—afadhali niifanye Jumapili ijayo, na Jumapili ijayo asubuhi.

¹⁵ Naye Ndugu Neville alisema, “Mbona usitoke tu uende ukawasalimie watu, na kuzungumza nao kwa dakika chache tu?”

¹⁶ Nikasema, “Ndugu Neville, hata sijaifungua Biblia yangu, karibu sijaifungua.” Nikasema, “Mimi...”

¹⁷ Yeye akasema, “Vema, toka uende ukawaambie jambo fulani.” Na, Dada Neville, si—si—sijui jinsi unavyofanya jambo hilo. Yeye ni mtu anayejua kushawishi sana. Lakini wakati...

¹⁸ Mimi sipati nafasi ya kusema jambo hili wakati mahali hapa pamejaa watu kabisa, na wamesongamana, na kila kitu, bali ninamshukuru Mungu sana kwa mchungaji kama Ndugu Orman Neville. Mwaminifu, mwaminifu tu anavyoweza kuwa, kwa Huduma, na huwezi kumsikia akinung'unika. Mimi huketi kule nyuma...Nilikuwa na nusu saa nzuri ya kuzungumza naye wakati nilipokuwa ninafurahia Ndugu Mann, na kwa hiyo nitamwambia mambo zaidi juu ya jambo hilo tutakapofika Colorado mwaka huu. Kwa hiyo tulipokuwa tukiufurahia

ujumbe wake, basi nilikuwa na mazungumzo mazuri na Ndugu Neville. Nikasema, “Hata sipati kuwaambia watu juu ya mchungaji wetu mzuri.” Nikasema, “Je! watu wanakutenda mema?”

Kasema, “Haiwezi kuwa vizuri zaidi.”

Nami nikasema, “Vema, hilo ndilo jambo ninalofurahia kusikia.”

¹⁹ Wakati mchungaji ameridhika, na watu wameridhika, inafanya kanisa zuri kweli, halafu Mungu ameridhika. Nami nafikiri, kuwaona wameridhika pamoja, hasa sana katika siku hii ya Ujumbe ambao tunabeba, nafikiri jambo hilo linaonyesha kuendelea kwa Ujumbe pamoja na watu na Mungu. Mnaona?

²⁰ Nami ninashukuru sana kwa ajili ya Ndugu Orman Neville, na mke wake mwema pamoja na jamaa yake. Nami naomba ya kwamba Mungu atawaweka wawe waaminifu Kwake na kwa Huduma. Na kama ikimpendeza, naomba tuwe tumesimama hapa Maskanini Bwana Yesu atakapokuja kwa ajili yetu, mnaona, kutuchukua katika Kunyakuliwa. Tunatumaini ya kwamba sisi wawili ni wazee sana, Ndugu Neville, hata mmoja atakuwa amemkumbatia mwingine kwa mkono, huku tumesimama pale kwa fimbo zetu, tukiwa tungali tunajaribu kushikilia. Mnaona? “Ndipo tutabadilishwa, katika dakika moja, katika kufumba na kufumbua.”

Ndipo mavazi haya ya mwili yataanguka,
Kisha tuinuke na kunyakua zawadi ya milele
Na kupaza sauti huku tukipita hewani,
“Kwa heri, kwa heri,” saa tamu ya maombi.
Tumesonga mbele kuelekea upande wa juu.

²¹ Mmesikia juu ya kuponywa kwa Ndugu Coomers na Bwana, nasi tunashukuru sana kwa jambo hilo. Mambo mengi sana. Kwa hiyo ninashukuru kuwa hapa asubuhi ya leo. Nami nikafikiri, badala ya . . .

²² Mimi daima ninakuja hapa na somo fulani, na kuzungumza. Nilifikiri ningekuwa tu asubuhi ya leo. Nami nikasema, “Ndugu Neville, nitaangalia ile saa ya ukutani kwa makini sana, na labda niwaache watu wafumukane kwa wakati mzuri, nami nizungumze nanyi tu kutoka kwenye moyo wangu, dakika chache; mambo tu, ambayo hatuna budi . . . La, wao hawayanasi ama cho chote kile, kwa hiyo tutafanya ushirika wakati kuna watu wa kanisa tu hapa, mnaona, sisi tu pamoja.

Kwa hiyo hebu na tuombeni.

²³ Yesu Mpendwa, tunakushukuru Wewe kwa majaliwa tuliyo nayo ya kukutanika pamoja hapa. Na, loo, nilipokuwa nikiyaangalia Maskani haya mapema asubuhi hii, baada ya usiku wa manane, nilipopitia hapa, nilifikiri juu ya jinsi Wewe ulivyoyatetea.

24 Nami nafikiria juu ya kile kidimbwi cha kale kilichokuwa hapa, na majani makubwa ya kale yaliyosimama, karibu kabisa na mahali mimbara hii ilipo. Kama mvulana mdogo, ni—nilisimama hapa. Bw. Ingram alisema tungeichukua ploti hiyo kwa fedha kidogo tu, na tutangulie kulipa kitu kidogo; na hakuna fedha, hakuna dhamana, ama cho chote kile cha kutoa, ila tu kujaribu. Jinsi ambavyo hiyo hapo, thamani yake kamili ilikuwa kidogo zaidi ya dola elfu mbili; tukiwa na miaka ishirini ya kuzilipia.

25 Na sasa, Bwana, iangalie sasa! Na ilipokuwa katika uchanga wake, ingali imekaa kwenye shimo hapa, maji yanaingia mle; jinsi Wewe ulivyotuahidi, kwa Neno: “Mimi Bwana nimeipanda, nitaimwagilia maji usiku na mchana, asiye mtu akaipokonya katika mikono Yangu.”

26 Wakati ule ule, watu walisema, “Katika muda wa miezi sita, itafanywa gereji.”

27 Bali maelfu ya watu kweli wamempata Kristo hapa madhabahuni. Nayo haya Maskani, mahali pa kubatizia daima...Watu wamebatizwa katika Jina la Bwana Yesu; wakiliitia Jina Lake, wakioshwa dhambi zao. Mamia ya waliolemaa, walioteseka, vipofu, vilema, viwete, walioliwa na kansa, wametembea wakaondoka toka kwenye jukwaa hili; wakaja, wakifa, wanaume kwa wanawake, wavulana kwa wasichana, nao wakaondoka wakaenda kuishi maisha mapya, wakiwa na mwili mpya miilini mwao, na wakitembea tena; wanaacha viti vyao vya kusukumia wagonjwa, mikongojo, na kadhalika. Ee Mungu, miaka thelathini ya utumishi!

28 Baba, nakumbuka ile asubuhi ambayo tulikuwa tumeweka jiwe la pembeni. Nawe ukanipa ono huko, ukionyesha mahali hapo, pamejaa na kusongamana watu, mahali pazuri pembeni; ni—nilijua ya kwamba jambo hilo halingeweza kushindwa. Kwa hiyo nakushukuru kwa mambo haya yote.

29 Wengi wao tayari wamepiga vita vizuri, na kuumaliza mwendo, kuilinda Imani; wamekaa kule ng'ambo, wakingoja, wakipumzika sasa kutoka kwenye kazi zao, na matendo yao yakifuatana nao; wakingoja ile saa baragumu itakapolia, nao wapate kufufuka tena katika maisha mapya, mwili mpya. Wengi wao ni wazee na wanatetemeka, wengine ni vijana, umri wa makamu, na kadhalika. Bali Jina Lako lisifiwe kwa ajili ya wote.

30 Sasa tunasimama hapa tena, mbele ya wa—walio hai na waliokufa. Naomba ya kwamba Wewe utayatia mafuta Maneno Yako asubuhi hii. Sijui neno moja la kusema, bali naomba ya kwamba Wewe utanipa hilo, jambo ambalo Wewe umetenda daima, Bwana.

31 Mbariki mchungaji wetu, Ndugu Neville, mkewe. Wabariki wadhamini, halmashauri ya mashemasi, kila mshiriki wa ule

mwili. Jalia, sote pamoja, tuishi namna hiyo katika maisha haya, ili kwamba katika maisha yajayo tutakuwa na Uzima wa Milele.

³² Tusaidie asubuhi ya leo tuchukue masahihisho kutoka kwa Roho na Neno, kusudi tupate kujiandaa tunapoondoka milangoni asubuhi hii, tumeazimia katika mioyo yetu kuishi maisha mema kuliko tulivyoishi hapo nyuma. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

³³ Sasa, ni—nimefungua Biblia tu hivi punde hapa, na imekuwa dakika chache zilizopita. Mimi niko katika Ufunuo 3, kwa hiyo nitasoma tu hapa, juu ya—ya Ujumbe kwa Kanisa la Laodikia.

³⁴ Nami nataka kutangaza, pia. Ndugu Neville alikuwa akiniambia hivi punde; Ndugu Parnell, kama nilivyopata kuangalia chini na kumwona ameketi hapa, yuko katika—katika ufufuo, upande huu tu wa Memphis. Kwenye—kwenye...ye yote wenu anajua mahali ile Wimpy, kibanda cha sambusa kilipokuwa, ana he—hema iliyopigwa pale, akijaribu kuileta miganda na kuona kama kuna waliopotea huko ambao walikusudiwa uzima, apate kuwavuta kwa huduma yake kwa Kristo. Naye aliifunga kwa ajili ya Jumapili, kwa ajili ya ibada kwenye Maskani, na—na huko ni kuwa mwaminifu sana kwa huyo ndugu. Nasi tunawataka mjue ya kwamba hizo ibada zitafunguliwa Jumatatu usiku unaofuata, juma lijalo. Nami najua nyote mmekaribishwa kwa furaha kumsikia Ndugu Parnell akileta ujumbe wake wa upendo wa Kristo.

³⁵ Na sasa hebu na tusome kutoka kwa Ufunuo sura ya 3, sehemu moja tu, kusema ya kwamba tulisoma Biblia. Kwa maana, yale ningesema huenda yakashindwa, bali anayosema Yeye hayatashindwa. Nami sijui nianzie wapi, nifanye nini, niende wapi, bali ninasoma tu Wakati wa Kanisa la Laodikia.

*...kwa malaika wa kanisa la...Laodikia andika;
Haya ndiyo anenayo yeye aliye Amina, shahidi aliye
mwaminifu na wa kweli na mwanzo wa kuumba kwa
Mungu.*

*Nayajua matendo yako...hu baridi wala hu moto;
ingekuwa heri...kama kwamba ungekuwa baridi au
moto.*

*Basi, kwa sababu una uvuguvugu, wala hu baridi wala
moto, nitakutapika utoke katika kinywa changu.*

*Kwa kuwa wasema, Mimi ni tajiri, nimejitajirisha,
wala sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe
u mnyonge,...mwenye mashaka,...maskini,...
kipofu,...uchi:*

*Nakupi shauri, ununue kwangu dhahabu
iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri;...mavazi
meupe upate kuwaa, ili kwamba aibu ya uchi wako*

isionekane; na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona.

Wote niwapendao nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidii, ukatubu.

³⁶ Mwajua, mahali fulani mle ndani, wakati nilipokuwa nikisoma, mimi . . . Kama mtanisamehe kwa dakika moja, ni—nilipata mahali fulani paliposikika pazuri kwangu mimi, nami sijui palikuwa wapi sasa. Pako hapa.

. . . nawe hujui ya kuwa wewe si . . . mnyonge, . . . mwenye mashaka, . . . maskini, . . . kipofu, . . . uchi.

³⁷ Loo, jamani, hiyo kwa namna fulani ni picha hapa ya kanisa la siku hii! Sasa, ni, na—nafikiri ya kwamba wakati huo wa kanisa hapa, ambao tunazungumzia habari zake . . . Hakuna budi, nina wakati wa kanisa unaokuja sasa katika vitabu. Bali kwa kuwa huo ni Wakati wa Kanisa la Laodikia tunaoshi, hebu tuangalie zile hali.

³⁸ Sitaki kuchukua somo lo lote ama cho chote kile, kwa sababu sisi si . . . tunazungumza tu vihi hivi, kama tunavyoona kuzungumza juu ya kile Bwana angetuongoza kuzungumzia, bali kitu ambacho kingetusaidia.

³⁹ Hebu tufikirie juu ya Wakati wa Kanisa la Laodikia na hali yake leo. Nijuavyo mimi, sioni kizuizi cho chote, kwa wakati huu, cha Kuja kwa Bwana Yesu, nje ya kuwa tayari kwa Kanisa. Nafikiri moja ya zile—zile nabii . . .

⁴⁰ Jana, tukija huku kwa gari, tuliliendesha siku mbili, kutoka Tucson, hapa, maili elfu mbili kabisa, mimi na Billy. Na kwa hiyo sisi, sasa, hiyo haikuwa kuvunja sheria yo yote ya mbio za magari. Tuliendesha sawa. Niliketi pale, kama yeye anaendesha, nami ni—kakunja—nikakunja ngumi zangu kama bunduki ya marissi yenye nyundo nyuma. Ninamwona anapitisha huo; nikasema, “Ngoja kidogo, ewe mvulana.”

Naam, tunaambiwa, “Mpeni Kaisari yaliyo ya Kaisari.”

⁴¹ Ndipo tukashuka hapa jana usiku, msichana mdogo amelala barabarani, ana kama umri wa miaka mitatu; mama yake amekufa upande wa pili wa handaki. Mvulana fulani mlevi, akiya kutoka R.O.T.C., ana umri wa miaka kumi na minane, akienda mwendo wa maili mia moja ishirini kwa saa, upande wa kushoto wa barabara, akauawa. Nami nafikiri alikuwa anakufa, yeye pia. Basi ungeweza kutambua ilikuwa ni nini.

“Mpeni Kaisari yaliyo ya Kaisari.”

⁴² Watu wasio na hatia wakifa. Msichana mdogo wa miaka mitatu alipoteza maisha yake, kwa maana askari fulani aliyelewa, mnaona, akiendesha gari kwa mwendo wa maili mia moja na ishirini kwa saa, alivyokadiria, upande usio sawa wa barabara. Akipanda kilima, kisha akashuka mbio moja kwa moja, naye akawaua wote pale pale pamoja. Mimi . . . Yeye

alikuwa anakufa, naye pia. Kwa hiyo basi unaweza kuona, hata ingawa hao wasio na hatia walifanya hivyo. . .

⁴³ Sasa mvulana huyo ana hatia ya mauaji ya kinyama. Mnaona? Nafikiri kama mtu angeshikwa barabarani, akinywa, anapaswa kufungwa miaka kumi, kabisa, kwa mauaji yasiyostahili, ya makusudi; mtu ye yote, kwa maana yeye. . . mtu ye yote.

⁴⁴ Sisi, hatutafanya jambo lo lote jema kwa siasa. Zimeoza. Wazo la Mungu la kuwa na mfalme, mfalme mwenye haki, ni sawa. Bali siasa kwa urahisi husambaa, unaweza kununua kitu cho chote; kudanganya, kusema uongo, kuiba, cho chote kile. Kama nilivyosema Jumapili chache zilizopita: basi angalieni mahali mlipo, mnaona, si kitu ila tu rundo la upotovu wa kila kitu. Bali mfalme mwenye haki anaweza kufanya sheria zake mwenyewe. Nawe unaweza kumuua mtu; unamjua mwanasiasa mzuri, hilo ni sawa, utaachiliwa. Mnaona? Na kwa hiyo, ni, hilo—hilo. . .

⁴⁵ Demokrasia ni wazo zuri, bali halitafaulu. Kama tu ukomunisti, vitu vyote shirika; linasikika ni jambo zuri, bali halitafaulu. La. Ile njia ya Mungu ya kuwa na mfalme, kama Daudi alivyokuwa, ilikuwa sawa, nawe una nia moja iliyowekwa kule. Kama kiongozi mmoja na kundi la bata, na kadhalika, huwezi kuchukua wawili ama watatu wao. Kisha, unawatatiza wote pamoja, unatokea na wazo la namna yo yote.

⁴⁶ Kwa hiyo tunaona hizo hali, leo, zikiwa tayari kwa Kuja kwa Bwana.

⁴⁷ Lakini, wakati mimi na Ndugu Neville, na hawa ndugu wengine wanajaribu kulichunga kundi, nina kitu fulani niani mwangu sasa, ambacho kinakuja, ambacho huenda tukazungumzia habari zake.

⁴⁸ Hicho ni kwamba, nilipata barua juzijuzi kutoka kwa bibi mzuri. Sikuipata; ilipitia kwa mtu mwingine. Naye hakika alikuwa akinirarua vipandevipande, ama anajaribu kufanya hivyo. Alikuwa anasema, “Je, uliwahi. . . Kwa nini nyinyi Wafanyi Biashara Wakristo msifanye kitu kumkomesha Ndugu Branham?” Kasema, “Maana ametoa kitabu hiki sasa kinachoitwa *Wakati wa Kanisa la Laodikia*, anatoa vingine zaidi.” Kisha kasema, “Yeye kweli anayararua mafundisho ya dini ya Kipentekoste vipandevipande.” Kasema, “Sasa anasema kwamba ushuhuda wa kwanza siyo kunena kwa lugha.” Kisha kasema, “Halafu, yeye anawapinga wahubiri wanawake.” Na huyu alikuwa mhubiri mwanamke. Na wavulana wake, baadhi ya marafiki wazuri sana nilio nao ulimwenguni. Mnaona, wao ni miongoni mwa marafiki wazuri sana nilio nao. Naye akasema, “Sasa. . .”

49 Na mtu huyu na mkewe, nilikuwa nikila kifungua kinywa pamoja nao; wakasema, “Ndugu Branham, angalia hii. Ungeweza kuliwazia?” naye katoa barua.

Nikasema, “Vema, dada, ni kwamba tu yeye hafahamu.”

50 Hao wavulana waliniambia ya kwamba mama yao alikuwa mhubiri mwanamke, na kwamba yeye hakukubaliana na huu Ujumbe.

51 Na sasa yeye anasema humu ndani, yeye alisema, “Sasa yeye alisema, Wanawake hawapaswi kutwaa mamlaka juu ya wanaume.” Kasema, “Vipi kuhusu Fibi katika Biblia, yule msaidizi wa Paulo?”

52 Bila shaka, yeye alikuwa muuza bidhaa. Naye Paulo akawauliza hao watu... Unafikiri Paulo angesema, “Wanawake na wanyamaze katika makanisa, hawana ruhusa ya kunena,” halafu ageuke na kusema, “Naam, Fibi, msaidizi wangu katika Injili, atahubiri siku chache usiku”? Mbona, angepinga neno lake mwenyewe. Mnaona?

53 Kisha akasema, basi, juu ya yote, “Naamini ilikuwa Esta... alikuwa mmoja wa waamuzi katika Biblia.” Kasema, “Mwanamke alikuwa mwamuzi katika Biblia. Kama hayo si mamlaka juu ya mwanamume!”

54 Na huyu mfanyi biashara aliyeponywa papa hapa kanisani si muda mrefu uliopita, yeye alisema... Sasa, mkewe akasema, “Ndugu Branham, jambo hilo daima lilinitatiza.”

Nikasema, “Mbona, dada, jambo hilo lingekutatizaje?”

Kasema, “Vema, huyu hapa mwamuzi mwanamke.”

55 Nikasema, “Hizo ni siasa, si kanisa. Jambo hilo halina uhusiano wo wote na kanisa.”

56 Paulo akasema, “Hebu watii, kama inenavyo torati nayo.” Na torati haiwezi kumweka mwanamke kuwa kuhani; haiwezi kumweka. Hamjawahi kumwona kuhani mkuu mwanamke. Hamjawahi kumwona kuhani mwanamke, hakuna mahali po pote katika Biblia. Hamjawahi kumwona mhubiri mwanamke, katika Biblia. Hakika.

57 Wengine wao walikuwa manabii wanawake, na kadhalika; Miriamu na wengine wao. Na Esta... Mmoja wao alikuwa mwamuzi juu ya Israeli. Wakati mwingine walikuwa malkia juu yao, na kadhalika namna hiyo, mfalme na malkia. Baada ya mfalme kufa, ilimbidi malkia kuchukua mahali pake hata walipomchagua mfalme mwingine, na kadhalika.

58 Katika Tucson—katika Tucson, Arizona, tuna mwamuzi mwanamke pale mjini. Hiyo ndiyo sababu mji huo umechafuka sana. Nasi tuna... Mwanamke hana shughuli zo zote katika siasa. Hana shughuli zo zote katika... juu ya mamlaka yo yote kanisani.

⁵⁹ Mahali pake ni malkia wa mwanamume nyumbani. Nje ya jambo hilo, hana kitu. Nasi tunajua jambo hilo kuwa ni Kweli. Hamtampata. . . Najua jambo hilo linasikika la mtindo wa kikale, bali mimi ninawajibika.

⁶⁰ Nami najua ya kwamba, baada ya kuondoka kwangu kutoka dunia hii, hizo kanda na vitabu vitaendelea kuwepo, na wengi wenu ninyi watoto wadogo mtaona, katika siku zijazo, ya kwamba jambo hili ni Kweli kabisa, kwa maana nanena katika Jina la Bwana.

⁶¹ Sasa, tunashangaa jinsi gani mwanamke, ambaye ni mwanamke mzuri, naye amewaleta humu duniani kwa mume wake mwaminifu, mwanamume mzuri, baadhi ya vijana wazuri sana niliowahi kukutana nao, ni wanaume, ambao nimewahi kukutana nao. Na upesi tu, mara tu waliposikia Ujumbe, waliushika kwa dhati, asilimia mia moja. Naam, jambo hilo lingeweza tu kutukia kwa kuchaguliwa tangu zamani. Hivyo ndivyo tu linavyoweza kuja.

⁶² Sasa, swali ni kwamba, hapa. Nilikuwa nikifikiria jambo hilo, mnaona, sasa kwa nini Bwana alikuwa akinirudisha. “Wala unajua, wajua. . . Hujui; wewe ni uchi, mwenye mashaka, mnyonge, kipofu, wala hujui.”

⁶³ Kabla sijafikia mahali hapo, ningetoa mhitasari wa yale niliyosema siku chache zilizopita, hapa katika Ujumbe juu ya, naamini ilikuwa, *Mungu Wa Ulimwengu Huu*; ameyapofusha macho ya watu, hata wao kabisa wanamwabudu ibilisi katika ibada za kidini. Nyote mlipata jambo hilo? Nyote mlilifahamu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

⁶⁴ Halafu katika Ujumbe uo huo, nililileta lile somo, ambapo, mwanamke akivaaa nguo chafu, bila adabu, yeye anahukumiwa katika ile Hukumu kama kahaba wa mitaani. Hilo linasikika la kigeni sana.

Hebu niwachoree picha ndogo.

⁶⁵ Sasa, huyu hapa mwanasheria mjini, jamaa mdogo, tena ni mtu mzuri. Kwa mambo ya—ya kisiasa, nafikiri huenda yeye ni muungwana kama ye yote yule, siasa zake. Halafu yeye anaandamana na msichana ambaye anapendwa sana na watu. Wanapendana na kufunga ndoa. Wao wanahudhuria karamu zote na mambo makuu, tena wanakunywa pamoja. Hatimaye, mwanamke. . . Mwanamume ana nyumba nzuri. Anaishi katika mtaa wa ujirani mzuri. Yeye anawaziwa mema na watu. Lakini mwanamume. . . Wote wawili ni walevi. Mwanamke anavaa kaptura, anakata nywele zake, anajipodoa, na kila kitu ni cha zinaa namna hiyo, yeye. . . mwanamke mrembo akijionyesha mwenyewe. Vema, yeye daima haendi kanisani, hata kidogo, wala mmoja wao.

66 Kwa hiyo, anahama, jirani nao, anakuja mwanamke kutoka kanisa la Kibatisti ama la Kimethodisti, yeye na mumewe. Naam, mwanamke huyu. . .

67 Hebu tuifanye Mmethodisti, kwa maana Wamethodisti wanaingia kidogo zaidi katika ya utakatifu kuliko Wabatisti; wote ila Wabatisti wa Agano Jipya, wao wanaamini katika utakatifu. Lakini, kwa kawaida, Wabatisti hawautafuti utakatifu hata kidogo, mnaona. Wao hawaamini katika jambo la namna hiyo. Kwa hiyo basi, sasa, hebu tuifanye Methodisti kwa maana wao wanaamini katika utakatifu.

68 Halafu basi Mwanamke wa Kimethodisti anahama akawa jirani wa mwanamke huyu, mtaa ule ule. Mumewe ni. . . Hebu tuseme yeye ni mhasibu wa serikali, na, ama afisi fulani. Vema, mwanamke huyu Mmethodisti anamwangelia huyo mwanamke mwingine.

69 Na wakati mwanasheria huyu anapotoka nje ya mji. . . Jina lake ni Yohana; tuseme jina lake ni Yohana. Naam, msifikirie juu ya jambo hilo sasa. Mimi ninachukua tu majina ya kujibunia sasa. Na jina lake ni Yohana. Vema, alizoea kuambatana na Ralph. Na hilo ni jina la kujibunia, hayo yote, mnaona, ili kwamba tu mpate kufahamu hiyo hadithi, kuchora picha.

70 Vema, muda si muda unajua, kwenye karamu ya ulevi, Ralph anamkumbatia tena. Vema, mwanamke anapandwa na hamaki sana, kwa maana anapendana tena na Ralph, anafikiri. Ndipo, baada ya kitambo kidogo, Ralph anaanza kukutana naye. Naye anaweza kumdanganya Yohana, amfanyie jeuri. Naye anafikiri yeye ni kipusa mwerevu sana, kwa maana anaweza kuambatana na Ralph, huku ameolewa na Yohana. Mnaona, huyu mwanamke hata hana uadilifu wo wote, naye hafikirii cho chote juu ya jambo hilo.

71 Bali mwanamke huyu wa Kimethodisti amekuzwa katika hali nyingine. Yeye, angalao, anaenda kanisani, naye anafikiri ya kwamba mwanamke huyo ni mbaya sana. Mbona, anamwambia mumewe, anapokuja, "Namwona yule mwanamume akienda kule na kukutana naye. Na wakati Yohana ameondoka kwenda katika kesi mahali fulani, Philadelphia ama mahali fulani, yeye anamchukua kwenye gari lake, nao wanalala kule pwani. Nawaona wakija nyumbani; hata hawafungi pazia wakati mwingine, anambusu na kufanya mapenzi naye, baadaye. . . Loo, si hilo ni jambo baya sana," anamwambia mumewe. "Naam, yeye si kitu ila kahaba wa mitaani." Hiyo ni kweli, yeye ni mbaya kuliko kahabawa wa mitaani, kwa maana yeye ni mwanamke aliyeolewa. Mnaona? Naye, mwanamke huyu, mwanamke huyu Mmethodisti, anafikiri jambo hilo ni baya sana, yeye haendi kanisani.

72 Naam, mwanamke huyu Mmethodisi hangefanya jambo kama hilo. La, hashu. Yeye ni mwanamke mwadilifu. Na jambo

lingine, yeye hangegusa wiski hata kidogo, kwa maana, kanisa la Kimethodisti, asilimia tisini ya miradi yao ni kupiga marufuku wiski, dhidi ya wiski. Kwa hiyo, wao wana mradi wa kupiga marufuku, na hao watu wa kanisa hilo la Kimethodisti hawaishi juu zaidi ya vile kanisa hilo linavyofundisha.

⁷³ Bali mwanamke yuyu huyu, mwanamke huyu wa Kimethodisti, anatoka nje, jioni moja, pamoja na mumewe, amevaa kaptura Jumapili, baada ya shule ya Jumapili. Yeye anakata nywele zake. Anajipaka rangi mdomoni, na hata anavuta sigara kidogo.

⁷⁴ Sasa, katika Neno la Mungu, wote wawili ni makahaba, bali huyu *hapa* ni “uchi, mwenye mashaka, mnyonge, kipofu, wala hajui.” Mmoja ana hatia kama tu yule mwingine, kwa kuwa, “Mwanamume anayemtazama mwanamke, kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake.”

⁷⁵ Na kama mwanamke huyu, sasa, yeye angesema, “Sasa ngoja kidogo tu, Bw. Branham. Nitakufahamisha, mimi si kahaba.” Dada yangu, labda kama ungepelekwa mbele ya Biblia, na uweke mikono yako juu Yake Mbele za Mungu, na kuapa kiapo kwamba umekuwa tu mwamini-f, mwaminifu kwa mume wako iwezekanavyo. Mwili wako ni wa mumeo, bali nafsi yako ni ya Mungu. Kuna roho mchafu aliyekutia upako. Kama jambo hilo, kama sivyo ulivyo, basi wewe ni . . . Naweza kuthibitisha ya kwamba wewe ni mwenda wazimu kabisa.

⁷⁶ Ingekuwaje kwa nyanya yako kama angalitembea barabarani huku amevalia kaptura hizo? Wao wangelimweka katika hospitali ya wenda wazimu; alitoka nje bila nguo zake. Kuna kasoro bongoni mwake. Kama ilikuwa hivyo wakati huo, ndivyo ilivyo leo.

⁷⁷ Kwa hiyo inautupilia ulimwengu wote katika wenda wazimu. Kitu hicho chote ni wenda wazimu. Na umeingia kisiri sana hata watu hawajui.

⁷⁸ Basi, yeye ni kahaba? Si kwa mumeo, nadhiri ya mwili wake. Lakini, mbele za Mungu, yeye ana roho mchafu na wa kikahaba, ambaye anamfanya avalie namna hiyo. Naye yuko katika Wakati wa Kanisa la Laodikia, naye hajui ya kwamba anafanya jambo hilo. Mwanamke huyu asiye na hatia hajui ya kwamba Mungu atamhukumu kama kahaba. Haya basi.

⁷⁹ Ati umweleze? Huwezi kumwambia. Hakuna njia ya kumwelezea. Biblia ilisema, “Wao ni uchi wala hawajui.”

⁸⁰ Kama ungemwita kahaba, wewe binafsi, angekufanya ushikwe. Angekufunga. Mimi kamwe sineni kibinafsi juu ya mtu ye yote. Ninazungumza juu ya dhambi. Sisemi, “Kanisa fulani *hili*, Bw. Fulani kule, Kasisi Fulani, yeye ni . . .” La, la. Mimi husema kwamba, fundisho la hilo, mnaona, jambo lote pamoja. Mimi siwataji watu binafsi. Si watu binafsi. Ni utaratibu walimo ndani yake. Ni utaratibu wote wa ulimwengu.

⁸¹ Ndugu George Wright anayeketi hapa ni. . . Yeye ana umri wa miaka sabini na mitano ama sabini na minane, nafikiri. Unafikiri ingekuwa je kama ungalienda kumwona Dada Wright siku moja, naye angekuwa amesimama huku amevalia kaptura? Mbona, wewe kamwe, unge—ungemfanya huyo mwanamke afungwe. Hungalimuoa kamwe. Vipi kama kijana mwanamume ye yote katika siku hiyo angalifanya jambo hilo, jambo lile lile lingalitukia. Vema, kama ilikuwa dhambi na ni jambo lisilo halali wakati huo, ni jambo lile lile; bali watu wameingia kichaa.

⁸² Hebu niwatabirie jambo fulani, kabla tu halijatukia. Ulimwengu mzima unarundikana katika ukichaa, na utaendelea kuwa mbaya na mbaya na mbaya, hata watakuwa kundi la wenye kichaa. Na uko karibu kuwa namna hiyo sasa.

⁸³ Ungewazia mtu akiendesha motokaa huku amezima taa, upande mbaya wa barabara; jambazi, mtoto mdogo, anadhaniwa ametoka kwenye shule ya sekondari hivi punde, anawaua watu kadha. Jambo hilo linawakomesha? Mwingine anakuja moja kwa moja nyuma yake, akifanya jambo lile lile. Waweza kuwazia kijana mwanamume anayewazia mwenyewe. . . anayewazia jambo lo lote, akitoka hapa na kutenda wanavyotenda?

⁸⁴ Ungewazia msichana, na upeo wa utu uke, mrembo, ana maungo mazuri, umbo, sura, uso, mrembo; na jambo lile lile lake kuwa mrembo linaonyesha ya kwamba tuko katika wakati wa mwisho. Mnaona, yeye kwa jumla ameyaendea mambo ya ulimwengu, vitu vya ulimwengu na si uzuri wa utakatifu, utamu ndani ya nafsi yake. Nimewaona wanawake, upande wao wa nje haukuwa kitu cha kuangalia, bali zungumza nao wakati mmoja, wazungumzie kwa dakika chache, wao ni kitu fulani halisi ambacho huwezi kuachana nacho. Mnaona, urembo wa nje ni wa ibilisi, ni wa ulimwengu.

⁸⁵ Waangalie watoto wa Kaini, jinsi walivyoliendea jambo hilo. “Wana wa Mungu walipowaona hao binti za wanadamu ya kuwa ni wazuri, wakajitwalia wake,” na Mungu kamwe hakuwasamehe.

⁸⁶ Angalia, wakati hao wanawake wa Israeli wenye—wenye mikono yenye sugu, na nywele za nyuzinyuzi; wakati hao wana wa Mungu walipokuja wakipitia katika nchi ya Wamoabu, halafu wakakutana na hao wanawake warembo wenye nywele zilizotengenezwa vizuri, zenye kuvutia, na rangi nyingi usoni mwao, ama cho chote kile unavyoziita; na wakati hao wana wa Mungu walipowaona hao wanawake warembo sana, nabii wa uongo alisema, “Sote tu sawa.” [Ndugu Branham anagonga mimbarani mara sita—Mh.] Nao wakaoa miongoni mwao, na Mungu kamwe hakuwasamehe.

⁸⁷ Waliangamia jangwani. Kila mmoja wao alifia kule, bila tumaini, bila Mungu, nao wamepotea Milele; wamelaaniwa milele, ingawa walikuwa wameuona wema wa Mungu, ingawa

walikuwa wamenywea chemchemi isiyokauka. Walikuwa wameunywea mwamba uliopigwa. Walikuwa wameiona ile nyoka ya shaba ikifanya miujiza. Walikuwa wamepitia chini ya ubatizo wa Musa katika bahari. Walikuwa wameuona mkono wa Mungu. Walikuwa wamekula chakula cha Malaika, nao walikuwa wamefanya mambo hayo yote. Bali walioa, wakawaacha wanawake wawaingize, na kuoa kati yao. Si kufanya uzinzi, kuoa tu kati yao; Mungu kamwe hakusamehe jambo hilo.

⁸⁸ Hiyo ndiyo mara ya pili ilipotukia. Sasa hapa tuko kwenye mara ya tatu, ni danganyifu sana kuliko hapo awali.

⁸⁹ Najua jambo hilo ni gumu. Nami mara nyingi nimeshangaa, katika njia nyingi, itakuwaje basi? Kwa nini inanibidi kuwazungumzia watu kwa busara hivi? Nini kinasababisha jambo hilo? Na hata hivyo, naona, kama si Mungu, hakungekuwako na mtu ye yote, hakuna mwanamke angeketi na kunisikiza. Bali wao wanarudi, maana kuna mtu aliye na nanga ya Kweli pale, ambaye anajua ya kwamba jambo Hilo ni kweli. Haidhuru, wao wanajua jambo Hilo ni kweli. Sasa angalia linalotukia. Najua ni gumu.

⁹⁰ Ni kama tu vile kama daktari alikupa dawa, nawe ukataa kuinywa, basi usimlaumu daktari kama ukifa. Na hii ni kama dawa. Vipi kuhusu watu hawa ambao daima hudai kwamba mimi ni mchukia wanawake?

⁹¹ Mnaona, angalia tu jinsi wanawake wanavyotenda, nami nitakuonyesha mahali kanisa lilipo. Uadilifu wa wanawake uko katika Laodikia, katika ulimwengu, kimwili, “uchi, wenye mashaka, vipofu, wala hawajui,” ha—hao watu, wanawake wa ulimwengu. Na kanisa liko katika hali ile ile. Angalia mambo ya kawaida yakiwa mfano wa ya kiroho, moja kwa moja, kila wakati. Naam, siku moja kwenye ile Hukumu. . .

⁹² Najua si jambo linalopendwa na watu kulisema. Na kama mtu hajachaguliwa kulisema, afadhali usiliseme; maana unaigiza, halafu utaingia shidani, kweli kabisa.

⁹³ Sasa angalia. Kweli mimi, inaonekana kama, katika nyakati zingine, nilikifungua kinywa cha mwanamke nikamwaga Dawa kinywani mwake, halafu nakishikilia kinywa chake kwa mikono yangu, naye ataitema kila wakati. Vipi kama daktari alifaya hivyo kwa mgonjwa, halafu huyo mgonjwa akafa kwa kuwa walikataa kuimeza hiyo dawa? Kwenye ile Hukumu, wakati mambo yote kama kukata nywele na kuvalia kaptura na . . .

⁹⁴ Mimi ninajenga tu. Ile saa imekaribia wakati mtakapoona jambo fulani likitukia, wakati jambo fulani litatukia. Na mambo haya yote ya utangulizi yamekuwa tu yakiweka msingi kwa ajili ya Ujumbe mfupi, na wa haraka ambao utatikisa mataifa yote.

⁹⁵ Sababu ya mimi kuwa nawakemea wanawake, imekuwa ikikaaa hapa kwa ajili ya kitu ambacho unaweza kukipiga

moja kwa moja kichwani, nayo. Hata kujaribu kuwaambia yaliyo kweli. Nami ninashikilia mkono chini namna *hii*, kama kwamba ni kinywa, nao wanaitema Hiyo. Basi ni nani anayeweza kumlaumu huyo daktari?

⁹⁶ Utasemaje, kwenye ile Siku ya Hukumu, wakati sauti ambazo zimelikemea jambo hilo, zitaicheza hiyo sahani ya santuri tena moja kwa moja mbele ya hao watu? Basi wao wataiepukaje?

⁹⁷ Wanaitema kupitia vidole vyako. Wanamwaga nyingine chini, halafu hatimaye wanavitikisa vichwa vyao na ku-...?... kurudi, wanarudi, hawatafanya jambo hilo. Hata hivyo, unarudi tena na kuimwaga ndani tena. Basi ni nani mwenye hatia? Si daktari, si ile Dawa, bali ni msimamo wa huyo mtu. Hiyo ni kweli kabisa. Itakuwa siku ya kuchukiza sana, moja ya siku hizi, wakati kizazi hiki chenye dhambi na kizinifu kitakaposimama mbele ya Mwenyezi Mungu.

⁹⁸ Naona miaka yangu ikisogea, mabega yangu yakiinama; na, najua, miaka thelathini hapa kwenye jukwaa hii, naam, miaka thelathini na mitatu hapa kwenye huduma. Hayo ni maisha marefu. Hiyo ni miaka thelathini na mitatu ya huduma. Juto moja tu; ya kwamba sikuwa na miaka mia na thelathini na mitatu ya jambo hilo. Kwa maana hii ndiyo nafasi ya mwisho nitakayowahi kuwa nayo, wakati niko hapa kama mwanadamu, kuihubiri Injili. Mungu na anisaidie kusimama nikiwa mwaminifu sana iwezekanavyo, kwa Neno hilo, na kusema vile tu Yeye alivyosema.

⁹⁹ Ni nini kilimfanya yule mwanamke wa Kimethodisti... Ungewezaje kamwe kumwelezea Hilo? Huyu hapa, kwenye huo Wakati wa Kanisa la Laodikia.

¹⁰⁰ Sasa tutamchukua mwanamke wa Kipentekoste. Yeye hangevaa kaptura, vipodozi, ama kukata nywele zake, bali anamwangelia huyo Mmethodisti, aseme, “Mwangelie mwanamke yule akifanya *hivi na vile!*” Tuseme huyo mwanamke havai kaptura, bali yeye anasema...naye ana nywele zilizokatwa. Mnaona?

¹⁰¹ Jinsi unavyopanda juu katika Mungu, ndivyo kitu hicho chote kinavyoonekana chenye dhambi. Halafu wakati mwingine, katika maombi, unaweza kuwazia, wakati Roho Mtakatifu anapokupeleka kwenye kiwango fulani, ndipo kitu hicho chote kinaonekana kimejaa mchafuko. Kisha unaposhuka chini tena, unaonekana kama kwamba wewe ni, kwa watu, wewe ni mlaghai, ya kwamba wewe ni—wewe si kitu ila mzee mkali. Wewe ni mpumbavu, kwa maana unasimama kama mzee mwenye kinyongo na daima unawakemea watu. Bali kama ukiwahi kupanda ukaingia katika viwango hivyo wakati mmoja, mahali unapoweza kuwa katika Uwepo wa Mungu (si kwa mshtuko, bali kwa kuinuliwa halisi na Roho Mtakatifu), kitu

hicho chote kimeandikwa, “ICHABOD.” Utukufu wa Mungu umeondoka kutoka kwenye mtindo huo wote wa kimadhehebu. Hiyo ni kweli. Hakuna hata moja yao hayo yaliyo sahihi.

¹⁰² Sasa hebu niwachoreeni duara ndogo. Kama ningalikuwa na ubao wa kuandikia . . . Bali nawatakeni mwangalie hapa. [Ndugu Branham anachora miviringo ifuatayo kwenye kitu fulani—Mh.] Nitachora mviringo mmoja namna *hii*, kisha nitachora mviringo mwingine ndani ya mviringo huo, hiyo ni miwili, halafu nitachora mviringo ndani ya mviringo huo. Hiyo ni miviringo mitatu, miviringo mitatu. Naam, hizo ni wewe.

¹⁰³ Huyu ni Mungu. Mungu katika utatu ni Mmoja, na bila utatu Yeye si Mungu. Yeye hawezi kudhihirishwa kwa njia nyingine yo yote.

¹⁰⁴ Wala wewe huwezi kudhihirishwa bila ya kuwa utatu ulio wewe, hivyo ni kusema: mwili, roho, nafsi. Bila moja ya hizo, wewe si mkamilifu. Mnaona? Usingekuwa na nafsi, ungekuwa si kitu wewe; usingekuwa na roho, hungekuwa kitu; usingekuwa na mwili, ungekuwa ni roho tu, si mwili.

¹⁰⁵ Kwa hiyo, Mungu amekamilika katika umoja wa utatu wa Mwenye Uhai mmoja; si umoja wa utatu wa *wenye hai*, bali Mwenye Uhai Mmoja katika umoja wa utatu. Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni Mungu mmoja na wa kweli aliyedhihirishwa. Mungu!

¹⁰⁶ Angalia hapa, hebu ngoja tu, na—naamini nililisoma dakika chache tu zilizopita. Sikilizeni hili.

*. . .kwa malaika wa kanisa la . . . Laodikia andika;
Haya ndiyo anenayo yeye aliye Amina, shahidi aliye
mwaminifu na wa kweli, mwanzo wa kuumba kwa
Mungu.*

¹⁰⁷ Mungu ni Muumba. Basi Yeye alipataje kuumbwa? Bali huu ni “mwanzo wa kuumba kwa Mungu.” Wakati Mungu, yule Roho, alipoumbwa katika mfano wa Mtu, huyo alikuwa Mungu akiumbwa; Mungu Muumba, Yeye Mwenyewe, akifanyika kiumbe. Mungu, Ambaye alifanya udongo, alifanya chokaa, aliyefanya shura, nuru ya ulimwengu, petroli, alichukua kitu hicho pamoja akajiumba Mwenyewe, hapo “mwanzo wa kuumba kwa Mungu.”

¹⁰⁸ “Yule Amina,” wa mwisho. Amina maana yake ni “na iwe hivyo.” “Mwisho wa Mungu,” wakati Mungu alipomaliza uumbaji Wake.

¹⁰⁹ Naam, ilikuwaje? “Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote, bali Yeye aliyetoka kwa Baba ndiye aliyemfunua.” Mnaelewa?

¹¹⁰ Aisee, hebu kidogo, hamna haraka. Hebu tufungue Wakolosai, kwa muda kidogo. Nilikuwa tu . . . Andiko limekuja niani mwangu. Hebu tufungue katika Wakolosai, Kitabu cha

Wakolosai, na tupate...Naamini ni sura ya 1. Sina budi kuliangalia hili, maana halikukusudiwa kabla hapa. Kwa hiyo nita-...Kama nilivyozea kuwa, nilipokuwa mhubiri kijana, niliweza kufikiria mambo haya [Ndugu Branham anakidata kidole chake mara moja—Mh.] sasa hivi tu, bali ninapokuwa mzee zaidi siwezi. Hebu tuanze kwenye aya ya 9, naamini. “Kwa sababu hii...” Ni Paulo akiwaambia Wakolosai juu ya Kristo, kwamba alikuwa Nani.

Kwa sababu hiyo sisi nasi, tangu siku ile tuliposikia, hatuachi kufanya maombi na dua kwa ajili yenu, ... mjazwe maarifa ya mapenzi yake katika hekima yote na ufahamu wa roho;

Mwenende kama ulivyo wajibu wenu kwa Bwana, mkimpendeza kabisa; mkizaa matunda kwa kila kazi njema, na kule kuzidi katika maarifa ya Mungu;

Mkiwezeshwa kwa ...wote, kwa kadiri ya ile nguvu ya utukufu wake, mpate kuwa na saburi ya kila namna na uvumilivu pamoja na furaha;

Mkimshukuru Baba, aliyewastahilisha... ambaye alitustahilisha...kupokea sehemu ya urithi wa watakatifu...

Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake;

111 Sasa hapa tunapata sasa. Angalia.

Ambaye katika yeye tuna ukombozi kwa damu Yake, yaani, msamaha wa dhambi;

Naye ni mfano wa Mungu asiyeonekana, ...

112 Mnaelewa? Aya ya 15, Wakolosai 1:15.

...mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote.

113 Amina! Ati nini? “Mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote.” Hata iwe ni Malaika, hata iwe nini; Yeye ni mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote.

Kwa kuwa kwa Yeye vitu vyo—vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni au vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana...visivyoonekana; ikiwa ni viti vya enzi, kama ni usultani, ...enzi, ...mamlaka; vitu vyote viliumbwa kwa njia yake, na kwa ajili yake.

114 Na iwe cho chote kile; hakuna mwenye uhai mwingine! Angalia, “Na katika... Na hivyo basi yeye ni...”

...amekuwako kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikana katika yeye.

115 Iwe Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, hata iwe nini, “Yeye amekuweko kabla ya vitu vyote.” “Kabla ya vitu vyote vilivyo Mbinguni, duniani; vinavyoonekana, visivyoonekana, ama cho chote kile,” huyu Mwana wa Mungu alikuweko kabla ya vitu

vyote. Hiyo ni kweli? Sijali, ni viti vya enzi, usultani, cho chote kile; viti vya enzi vya Mbinguni, falme, hata iwe nini katika zile milki kuu za kimbinguni huko ng'ambo, katika Umilele mahali ilipokuwa; hata kama ilikuwa nini, Malaika, miungu, hata iwe nini, "Yeye alikuweco kabla ya vitu vyote." Amina! Hamwezi kumwona? "Yeye alikuwako kabla ya vitu vyote; navyo viliumbwa na yeye. Yeye. . ." Aya ya 17.

Naye amekuweco kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikana katika yeye.

¹¹⁶ Hakuna kitu kinachoweza kuifanya itende kazi ila Yeye. Hata ikiwa ni Mungu Baba, Mungu Roho Mtakatifu; kama ni Malaika, enzi, mamlaka, usultani; cho chote kile, vyote vinatenda kazi Kwake. "Vitu vyote hushikana katika Yeye." Yeye!

Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo—naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu (hiyo ni kusema, afufue wale aliokuja kuwakomboa); ili kwamba awe mtangulizi katika yote.

¹¹⁷ "Apate kuwa *mtangulizi*," mnajua maana ya hilo? Hiyo ni kusema, "mkubwa wa yote." Yeye ni mkubwa wa vitu vyote vilivyopata kuumbwa; kila Malaika, kila mwenye hai, kila—kila kitu kilichopo. Yeye ni mkubwa wa vitu vyote. Ni Kiumbe gani Hiki? Anaweza kuwa Nani? Mkubwa wa vitu vyote! "Akiisha kufanya amani. . ." Hebu tuone, kwa muda kidogo. Mtanguli-. . .

Kwa kuwa katika yeye ilimpendeza Baba kwamba utimilifu wote ukae;

¹¹⁸ "Utumilifu wote wa mambo yote." Utumilifu wote wa Mungu, utimilifu wote wa Malaika, utimilifu wote wa wakati, utimilifu wote wa Umilele; kila kitu kilikaa ndani Yake. Huyu ni Jamaa huyu.

Na kwa yeye kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake, akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake; kwa yeye, ikiwa ni vitu vilivyo juu ya nchi, au vilivyo mbinguni.

¹¹⁹ Huyu hapo Mwenye Uhai mkuu yule tunayezungumza habari Zake, "Mwanzo wa kuumba kwa Mungu."

¹²⁰ Sasa, sasa hilo, Kanisa, kwamba kusudi Lake lote lilikuwa Kanisa. Sasa tunaingiaje katika Kanisa hili? "Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja," lile Kanisa, Mwili wa Kristo. Haliwezi kushindwa.

¹²¹ Naam, hivi ndivyo inavyotukia. Sasa angalieni jambo hili, picha ndogo tu ya mfano hapa. [Ndugu Branham tena anaonyesha mchoro wake wa duara tatu—Mh.]

¹²² Sasa, mtu huyu wa nje ni mwili. Huo ndio tunaouangalia; ule tuuonao. Nao una viingilio vitano kwenye mwili huo. Na mtoto

ye yote wa shule ya msingi, kama vile mimi, angejua kuna hisi tano zinazoutawala mwili; kuona, kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia. Bila ya hizo, huwezi kuugusa huo mwili. Hiyo ndiyo njia tu uliyo nayo kwenye huo mwili; kuona, kuonja, kugusa, kunusa, kusikia; unakiona, unakionja, unakigusa . . . Naam, huyo ndiye yule mwovu, upande wa nje.

¹²³ Sasa, ndani ya huo kuna roho fulani, ambayo ndiyo wewe unakuwa unapozaliwa duniani na pumzi ya uhai inapuliziwa ndani yake. Roho hiyo ni ya asili ya kidunia kwa sababu haikutolewa na Mungu, bali (ilitolewa) iliruhusiwa na Mungu. Sasa mmepata jambo hilo? Kwa kuwa, kila mwana aliyezaliwa ulimwenguni, “amezaliwa katika dhambi, akaumbika katika uovu; akaja ulimwenguni akisema uongo.” Hiyo ni kweli? Kwa hiyo, mtu huyo, mle ndani, ni mwenye dhambi, kwanza. Naam, lakini . . .

¹²⁴ Naam, ina milango mitano. Na hiyo milango mitano . . . Sijui kama ningeweza kuitaja sasa hivi. Wakati ule . . . Kwanza, najua, ni wazo, dhamira, na upendo, chaguo . . . La. Dhamira, upendo, hoja . . . Kuna milango mitano kwenye roho. Huwezi kuwaza kwa mwili wako; huna budi kuwaza kwa roho yako. Huwezi kuwa na dhamira mwilini mwako. Hauna nguvu za akili hata kidogo; mwili wako hauna, kwa hiyo huna budi kuwaza kwa roho yako. Huna budi kuhoji. Huwezi kuhoji kwa mwili wako wa kawaida, kwa maana hoja haioni, haionji, haigusi, hainusi, ama kusikia. Hoja ni kile unachoweza kufanya akilini mwako. Kama umelala ama umezimia, mwili wako umelala pale umekufa, bali roho yako ingali inaweza kuhoji. Kuna hisi tano ambazo humtawala huyo mtu wa ndani. Na hizo . . .

¹²⁵ Sasa, kwa huyu mtu wa mwisho, ambaye ni nafsi, kuna hisi moja tu inayoitawala hiyo, na hiyo ni hiari . . . hiari ya kujichagulia ama kukataa.

¹²⁶ Na sasa sababu ambayo watu leo . . . Naam, msisahau jambo hili sasa, nanyi mtaon—mtaona kile Roho . . . ushahidi wa kwanza wa Roho Mtakatifu ni nini. Mnaona?

¹²⁷ Sasa, watu wanaweza kuishi katika roho huyu, na wanacheza katika roho. Wanapiga kelele katika roho. Wanaenda kanisani katika roho, nao kweli wanaweza kuwa na upako wa Roho halisi wa Mungu juu ya huyo roho, bali hata hivyo wapotee na wapagawe na ibilisi sana wawezavyo kuwa, wakiwa na roho huyo.

¹²⁸ Kwa sababu, angalia, hiyo ndiyo sababu hungaliweza kumwambia mwanamke huyo, alikuwa amevaa kaptura, alikuwa amekosea. Hungaliweza kumwambia kukata nywele zake ilikuwa makosa. “Vema, nywele zako zina uhusiano gani na jambo hilo?” Vema, zilikuwa nao kwa Samsoni. Mnaona?

¹²⁹ “Ye yote atakayeongeza Neno moja kwenye Hili, ama kuondoa Neno moja kutoka Kwake.” Huna budi kuwa na mkataa mahali fulani.

¹³⁰ Sasa, kwa mfano, kama nilikuwa M—M—M—Mbatisti, nawe ukashuka ukaniambia lazima ni—lazima nibatizwe katika Jina la Yesu Kristo; liko katika Biblia. Vema, muda si muda, ningesema, “Nitamuuliza mchungaji wangu.”

¹³¹ Nami namwendea mchungaji; yeye aseme, “Loo, hilo ni jambo fulani la huko nyuma, unaona. Naam, unaona, sisi Wabatisti, haya ndiyo tunayoamini; tunaamini ya kwamba tunapaswa kuzamishwa majini katika vyeo vya ‘Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.’ Hivyo ndivyo kanisa lote limetenda hilo. Tangu John Smith alipolanzisha, hivyo ndivyo linavyotendwa.” Vema, hilo ndilo neno lako la mwisho. “Fuata aliyosema jamaa huyo!”

¹³² Vipi kama wewe ni Mmethodisti, na kunyunyizia ndiyo desturi yenu, nawe unaambiwa huna budi kuzamishwa majini? Mnaona ninalomaanisha? Unarudi kwa mchungaji wa Kimethodisti, naye atamwandikia na kumuuliza askofu, kama kadha alisema fulani juu ya jambo *hili*. “Lakini sisi, kanisa la Kimethodisti, tulianzishwa miaka mia tatu ama mia nne iliyopita, huko Uingereza, na John Wesley, na Whitefield, na hao wengine wote kule, na Asbury. Sisi tulianzisha mkataba huu, tukimfuata John Wesley, ya kwamba inatubidi kunyunyiziwa maji, kwa maana ni msisim-... utaratibu wa nje tu. Nasi tunafikiri kunyunyizia maji ni kuzuri tu kama njia nyingineyo ile.” Kama wewe ni ninino halisi... Kama kanisa la Kimethodisti ndilo neno lako la mwisho, huo ndio umbali unaoweza kwenda.

¹³³ Kama wewe ni Mkatoliki... Nami nitakwambia, haiko kwenye Biblia kutokula nyama Ijumaa, na mambo haya yote kama haya, na Ukaristi Takatifu si mkate mwembamba, kwa maana ni Roho,” na kadhalika. Nawe unamwendea kasisi wako, na huyo kasisi anasema, “Hili hapa, limeandikwa moja kwa moja katika mkataba wetu.” Na kama kanisa ndilo neno lako la mwisho, hujali kamwe yale mtu ye yote anayosema. Hilo ndilo neno lako la mwisho.

¹³⁴ Ee Mungu, saidia jambo hili likolee ndani! Kwangu mimi, jambo lote ni makosa. Neno la Mungu ndilo mkataa. Lo lote Neno hilo lisemalo, basi hilo ni sahihi.

¹³⁵ Sasa, njia pekee hapa juu katika viwango hivi, ambapo ungeweza sikuzote kuwa ndani ya huyu mtu mdogo wa ndani; nawe huna budi kuchaguliwa kabla. Kwa maana ulikuwa pamoja na Mungu, wewe ni sehemu ya Mungu.

¹³⁶ Nilikuwa ndani ya baba yangu. Nilikuwa pia katika babu yangu, na babu ya babu yangu. Kwa mbegu, nilikuwa ndani yake.

¹³⁷ Nami nilikuwa katika Kristo. Wewe ulikuwa katika Kristo kabla ya kuwekwa misingi ya dunia. Yeye alikuja kuwakomboa walio Wake, walio Wake waliokuwa katika Yeye. Haleluya! Watoto Wake waliokuwa ndani Yake!

¹³⁸ Yeye hakuja kamwe ku—kuwaokoa watoto wa ibilisi. Wao daima hawatajua jambo Hilo. Nao ni wajanja sana katika njia zao za masomo ya akilini, hata huwezi kujilinganisha nao kamwe. Huwezi kuwashinda katika mazungumzo. Lakini, kwa imani unaliona Hilo.

¹³⁹ Naam, sayansi haihitaji imani yo yote. Sayansi huthibitisha wanayozungumzia. Haihitaji imani.

¹⁴⁰ Kasisi wa Kikatoliki atakwambia, “Angalia jinsi gani kanisa Katoliki limestahimili kwa muda mrefu. Angalia jinsi gani lilivyoyastahimili mateso ya upagani kwa muda mrefu.”

Kanisa la Kimethodisti linasema, “Angalia hapa ni muda mrefu vipi. . .”

¹⁴¹ Nimeona kanisa. . . zungumza kuhusu ishara ya unafiki; nilipokuwa ninashuka nikija barabarani jana, niliona. Ilisema, “Kanisa la Kristo, lililoanzishwa AD 33.” Halijatimiza miaka mia moja bado, mnaona, madhehebu hayo. Loo, jamani! “Fundisho la mitume”? Karibu halina kitu. Hao ndio Mafarisayo wa siku hii; hawana Roho, hawana. . . Nawe huwezi kuwaambia; huwezi kuwazungumzia; huwezi kuhojiana nao.

¹⁴² Kwa sababu, tunaenda mbele zaidi ya hoja. “Usizitegemee akili zako.” Imani haihoji kamwe. Imani huamini Hilo.

¹⁴³ Wao wanasema, “Naam, angalia hapa, unaamini tunapaswa kufanya mambo haya kule nyuma? Upuzi! Hayo. . .”

¹⁴⁴ Bali Biblia ilisema hivyo. Siwezi kueleza jinsi inavyotukia, lakini hutukia. Mungu alisema hivyo. Kwa hiyo si lazima. . . Mimi siwezi kukwambia jambo lo lote juu yake. Imani haelezi jambo Hilo. Ulijua hivyo? Imani huliamini tu.

¹⁴⁵ Yesu alimwambia Nikodemo, kutoka Bara- . . . baraza la ekumenia la siku Yake; alimjua usiku, kasema, “Bwana, tunajua ya kwamba Wewe ni Mwalimu aliyetoka kwa Mungu, kwa kuwa hakuna mtu angeweza kufanya mambo unayofanya, isipokuwa Mungu yu pamoja naye.”

¹⁴⁶ Yeye akasema, “Amin, nakuambia, ‘Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi hata kuuona Ufalme wa Mungu.’”

¹⁴⁷ Kasema, “Mimi, mzee, niingie katika tumbo la mama yangu, kuzaliwa?”

¹⁴⁸ Yeye akasema, “Sasa nitakwambiaje mambo ya Mbinguni, wakati hata hutaamini mambo ya duniani?” Mnaona?

¹⁴⁹ Kisha akasema, siku moja, “Msipoula mwili wa Mwana wa Adamu, mnywe Damu Yake, hamna Uhai ndani yenu.” Yeye hakuelezea jambo hilo.

¹⁵⁰ Hao mitume na wengineo wa siku hiyo, waliokusudiwa Uzima, waliojua jambo hilo. Kasema, “Wote alionipa Baba watakuja Kwangu. Jambo tu likupasalo kufanya ni kuifanya Sauti Yangu ijulikane; wao wanaijua, kwa maana kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu.” Na sauti ni neno lililotamkwa. [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.] “Wao wanaiamini Hiyo, hata hivyo. Si lazima wathibitishe lo lote kisayansi, ama kumuuliza Msadukayo ye yote ama Mfarisayo, ama cho chote kile, juu ya jambo hilo. Nilisema hilo, wao waliaimini, kwa maana kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu.”

¹⁵¹ Na *Hili* ndiyo ile Sauti ya Mungu kwa jinsi ya herufi, kwa maana *Hili* ndilo ufunuo wote wa Yesu Kristo, Agano la Kale na lile Jipya yakiwekwa pamoja. Amina. Haya basi.

¹⁵² Kwa nini? Mnasema, “Hawa ni watu wazuri. Nini kinachowafanya . . .” Kwa sababu, jambo moja, nguzo yao ya kujishikiza ni kanisa. Na humu ndani . . . Mnalikumbuka lile la Jumapili iliyopita, juma moja lililopita; ni wangapi waliokuwa hapa na kusikia somo juu ya *Waliopakwa Mafuta Katika Siku Za Mwisho*? Nafikiri ninyi nyote. Mnaona, wao wamepakwa mafuta. Roho zao zimepakwa mafuta, katika kiwango *hiki* cha pili.

¹⁵³ Sasa, mwanamke huyo wa kwanza anasema . . . La, hajali kamwe yale kanisa lisemayo, yale mtu mwingine ye yote aliyosema. Yeye ni kipusa mwenye akili. Ana elimu ya chuoni. Yeye angeitumia kwa mumewe, na kufikiri yeye ni mwerevu kwa kufanya jambo hilo.

¹⁵⁴ Mwanamke huyu mwingine ni “uchi, kipofu, wala hajui.” [Ndugu Branham anagonga mimbara mara mbili—Mh.] Loo, linasikitisha, bali hiyo ndiyo picha inayotuchorea Biblia. Naam, yeye huenda kanisani. Mwanamke huyo, labda afadhali huyo mwanamke angekuwa . . . Yeye anaishi maisha mazuri na masafi; hakuna neno dhidi ya jambo hilo. Mungu ndiye atakayekuwa Hakimu wa jambo hilo. Sijui; mimi si Hakimu.

¹⁵⁵ Mimi ni ninino tu . . . ninawajibika kwa yale anayonionyesha Yeye. Hivyo ndivyo walivyosema mitume. “Tunanena yale ambayo tunajua, yale tumesikia, yale tumeona.” Hayo tu ndiyo minayowajibika kwake. Hayo ndiyo tu unayowajibika kwake.

¹⁵⁶ Lakini sasa, mnaona, kama ungemchukua mwanamke yuyo huyo . . . Yeye aliishia wapi? Mnaona? Yeye alizunguka moja kwa moja. Alisikia, hapana shaka; akaifungulia redio, mara nyingi. Sauti ya Mungu imekuwa ikinena, mara nyingi. Vema, sasa, mnaona, anaingia katika madhehebu haya hapa, kabila fulani. Makanisa yote ni makabila. Kila kitu, hiyo ni kweli kabisa, ni vyumba vya kulala tu ambamo watu hukusanyika pamoja kama wafuasi. Naye anakuja hapa; vema, hapo panamfaa kabisa. Sasa ukianza kumwambia yanayompasa kufanya, hatakusikiza. Unamwonyesha katika Biblia; hatalisikiza Hilo.

157 Naam, ndugu yangu mpendwa, dada, jambo moja ama mambo mengine mawili tu kabla ya kufunga. Imebakia robo sasa, wakati wa kufumukana; dakika kumi na tano.

158 Sasa angalieni, nataka kuwaulizeni jambo fulani. Kwa nini mwanamke huyo hawezi kuona jambo hilo? Kwa nini hawezi? Kuhusu kuwa katika uzinzi kimwili, kwa mumewe, yeye hana hatia; hana jambo la kutubia. Yeye ni msafi tu kama alivyokuwa siku aliyozaliwa; hakuna mwanamume amemgusa.

159 Ninazunguma sambamba sasa, kwa huyo mwanamke, kwa kanisa. Yeye ni msafi jinsi alivyozaliwa. Vema, hivyo ndivyo kanisa lilivyo hasa, jinsi alivyozaliwa, lakini yeye “alizaliwa katika dhambi, akaumbika katika maovu, akaja...” Mnaona ninalomaanisha?

160 Sasa wewe mwambie ya kwamba ni vibaya kwake kukata nywele zake; Biblia ilisema hivyo. Ni vibaya kwake kuvaa hizo kaptura; Biblia ilisema hivyo. Yeye angesema, “Upuzi.” Kwa nini? Mkataa wake si *huku* chini, katika huyo mtu wa tatu, nafsi iliyochaguliwa tangu zamani na ikatumwa kutoka kwa Mungu. Bali mkataa wake uko kwenye madhehebu *hapa* nje, ambayo watu fulani wameunda nje ya Hili. Mnaona?

161 Lakini kama Neno la Mungu liko ndani ya hiyo nafsi, inasema, “Amina! Ninaliona.” Inakubaliana Nalo. Sasa angalia hapa. Kwa hiyo, mtu aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu...

162 Mnaona, huu *hapa* mwili wa nje. Naam, ninazungumza katika kusanyiko lilichanganyikana, bali ninazungumza kama mchungaji we—wenu, kama ndugu yenu. *Huu* hapa ni mwili, nao ni mnyonge, hauna budi... Maskini bibi fulani anatembea barabarani; kijana mwanamume fulani katika ujana wake, akiwa ana umri wa miaka kumi na saba, kumi na minane, ishirini, ishirini na mitano, thelathini, anatembea anatembea-tembea pale ndani... Naye huyu bibi kijana anakuja, akijinyonganyonga kila sehemu, mwili wake, akitembea kwa viatu vya visigino; huku amejibenua kifua mbele na kujibenua kiuno; nayo nguo imefika *hapa* juu ya magoti yake, ama amevalia kaptura. Mnajua Biblia ilisema yeye angetenda hivyo? Mnajua, Biblia ilisema ya kwamba hivyo ndivyo angetenda, jinsi angetenda mchafu sana.

163 Je! mlisoma hili hapa, *Reader's Digest* la mwezi huu, ya kwamba, “Wanaume na wanawake wa siku hii, wasichana wadogo, kutoka umri wa miaka ishirini ama ishirini na mitano, wanaingia ugumba,” ya kwamba unapitia katika mabadiliko ya maisha katika umri wa makamu, kulingana na sayansi, kati ya umri wa miaka ishirini na ishirini na mitano. Ilikuwa kwenye thelathini ama thelathini na mitano, katika kizazi changu. Katika kizazi cha mama yangu, mwanamke hakuvingia ugumba mpaka alipokuwa na umri wa miaka arobaini ama arobaini na mitano.

¹⁶⁴ Ni nini? Ni kupitia sayansi, na chakula, na vitu vilivyochanganywa mbegu, hivyo vimeupotosha mwili wote wa mwanadamu hata tumekuwa kundi la—la—rundo la uharibifu. Vema, kama mwili wa kawaida umeharibika, je! chembechembe ya akili katika mwili huo wa kawaida haijahiribika? [Ndugu Branham anapigapiga mimbarani mara nne—Mh.]

¹⁶⁵ Sasa angalia Roho, akifuatilia hilo. Utakuja wakati, katika Jina la Bwana, ambapo watu watashikwa na wazimu kabisa. Biblia inasema hivyo. Wao watapiga mayowe na makelele; vitu vikubwa mno na vyenye sura ya kutisha katika mawazo ya akili zao. Redio na kadhalika, vipindi vyetu vya televisheni, vinitengeneza. Kutakuwa na vitu kama chungu watakaoinuka juu ya nchi, ambao watakuwa na urefu wa miti kumi na minne; kutakuwako na nde—nde—ndege atakayeruka duniani, mwenye mabawa yenye upana wa maili nne ama tano; na watu wakiwaona, watapiga makelele na mayowe, na kuililia rehema. Bali itakuwa ni vile Vitasa. Ngojeni hata nitakapohubiri juu ya kufunguliwa kwa vile Vitasa.

¹⁶⁶ Angalia alivyofanya Musa katika mwili wa kawaida, si Roho, wakati Yeye aliposema, “Musa . . .” Mungu alimwambia Musa, “Ondoka uende kule,” kwa nabii Wake, “chukua kozi ya vumbi, itupe juu hewani kisha useme, ‘BWANA ASEMA HIVI, viroboto watakuja juu ya nchi.’” Hakukuweko na viroboto. Muda si muda, wakaanza kuona kitu fulani kikitambaa kijitini. Wakaangalia, kuna na kitu kingine. Na baada ya kitambo kidogo, walikuwa wamerundikana kwa kina kirefu hivi kwamba hungaliweza kuwavuka.

¹⁶⁷ Walitoka wapi? Mungu ni Muumba. Yeye anaweza kufanya anayotaka. Yeye ni mwenye mamlaka. Yeye angeweza kufanya nde—ndege ambaye angefikia—mabawa yake yangetoka upande mmoja wa dunia hata mwingine.

¹⁶⁸ Yeye alisema, “Na waje nzi, waifunike nchi nzima.” Hapakuwepo na nzi hata mmoja nchini. Muda si muda, maskini nzi wa kijani akaanza kuruka kila mahali. Jambo la kwanza, na kulikuwa na wanane ama kumi, kumi na wawili. Muda si muda, usingaliweza kuwavuka. Mungu, aliye Muumba, hudumisha Neno Lake.

¹⁶⁹ Ndipo akainyosha fimbo yake, kwa amri ya Mungu, akasema, “Na vyura waje wakaifunike nchi.” Nao vyura wakaja hata wakarundikana, marundo, na uvundo ulikuwa kila mahali, labda futi arobaini ama hamsini kwenda juu, za vyura. Walikuwa katika kabati la—la Farao. Walikuwa katika . . . geuza shuka, na kungekuwa na vyura mia tano chini ya hilo shuka, chini ya kitanda, katika chakula. Kila walikokwenda, kulikuwako na vyura, vyura, vyura. Walitoka wapi? [Ndugu Branham anagonga mimbara mara nne—Mh.] Mungu, aliye Muumba, ni mwenye mamlaka. Asemayo, Yeye atafanya!

¹⁷⁰ Naye alisema kutakuwa na vitu vyenye sura ya kutisha juu ya nchi. “Nzige wenye nywele kama za wanawake,” nywele ndefu, kuwatesa hao wanawake wanaokata nywele zao. “Meno kama ya simba; miiba kwenye mikia yao, kama nge; watawatesa watu, miezi.” Ngojeni tu hata tutakapofikia kufunguliwa kwa vile Vitasa na Mihuri, na hizo Ngurumo Saba, mtaona yatakatotendeka. Loo, ndugu, afadhali uende Gosheni wakati kungali na wakati wa kwenda Gosheni. Usujali huu wa nje.

¹⁷¹ Angalia hapa. Huyu hapa maskini bibi mmoja anayeshuka kwenda barabarani huku anajinyonganyonga; huyu hapa jamaa mdogo, macho yake yanaona jambo hilo. Yeye ni mfuasi wa kanisa. Ni Mpetekoste. Ni cho chote kile. Bali muda si muda, hakuna nguzo ya kujishikiza *mle* ndani. Bibi huyo atasema, “Alo.” Ana nywele zilizoviringana, na ana sura nzuri, kijana mwanamume mwenye mabega yaliyonyooka; labda alijaribu kuishi maisha mazuri. Mwanamke huyo anaanza kumwendea, hata mhubiri. Muda si muda . . .

¹⁷² Ni nini? Huu nje *hapa*, tamaa ya mwili; na roho iliyo *hapa* chini, ingawa ina upako, ikisema, “Usifanye hivyo, usifanye hivyo.” Lakini itafanya nini? Itazunguka moja kwa moja, ishike pale, hiyo hapo inaenda. Muda si muda, anajaribu kufanya miadi naye. Yeye ana hatia ya kufanya uzinzi, amguse asimguse.

¹⁷³ Lakini, mwana wa kweli wa Mungu aliyezaliwa mara ya pili! Amina! Huwezi kufanya jambo hilo wewe mwenyewe. Haiwezekani kabisa kwa—kwa mwanamume halisi kutembea mbele ya mwanamke namna hiyo, bila kitu fulani kutukia. Bali wakati kuna Kitu huko ndani; hicho Kitu kidogo kilichozaliwa mara ya pili *hapa*!

¹⁷⁴ Ingawa labda mtu huyo alikuwa amepiga makelele, akanena kwa lugha, akaruka, akacheza, cho chote kile, ana upako wa Roho; akafanya ishara zote na maajabu ambayo Mungu alisema *mle* ndani, kwa Roho Wake! [Ndugu Branham anagongagonga mimbara mara tatu—Mh.] Yesu alisema, “Wengi watakuja Kwangu siku ile, waseme, ‘Bwana, sijafanya unabiii katika Jina Lako? Sijatoa pepo katika Jina Lako? Sija-. . .’ Yeye akasema, ‘Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu.’” Uovu ni nini? Jambo unalojua unapaswa kufanya, wala hulifanyi. “Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu; hata sikuwajua ninyi.”

¹⁷⁵ Bali upande wa ndani wa mtu huyo, kama hiyo nguzo ndogo ya kujishikiza imo *mle* ndani, hiyo Mbegu ya Mungu iliyochaguliwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu; sijali ni jambo gani linalotukia, inamshikilia. Ni ya kudumu.

¹⁷⁶ Hiyo ndiyo sababu mwanamke huyo atavaa hizo kaptura. Yeye anahesabiwa kuwa kahaba, sawasawa na mwanamke anayefanya tendo hilo. Mnaona? Yeye hajui ya kwamba hiyo roho . . . Anajuaje? Mkataa wake.

177 Mkataa ni nini? Ni neno la mwisho. Mkataa ni amina. Ni mwisho wa mizozo yote, mkataa wako.

178 Na kama kanisa lako, kanisa la Kipentekoste, ambalo linakwambia kwamba, “Nywele ndefu na kadhalika ni ushupavu wa dini tu. Una tairi ya spea, upande wa nyuma wa kichwa chako,” na kadhalika, mambo kama hayo, mtu huyo amepagawa na ibilisi.

179 Kwa kuwa, Neno la Mungu lilisema, “Ni aibu kwa mwanamke kukata nywele nywele zake. Atakiaibisha kichwa chake.” Kama akimwaibisha mumewe, na mumewe ni Kanisa, na Kanisa ni Kristo, yeye ni kahaba wa kidini asiye na heshima; yu uchi wala hajui. Uchi! Biblia haikusema, “Kifuniko cha mwanamke ni nywele zake”? Si alipewa nywele zake ili ziwe za kujifunika?

180 Siku moja, kule ng’ambo katika ile Hukumu! Nimejaribu kutia dawa mle ndani, na kuishikilia kwa mikono yangu, nanyi mnaitema moja kwa moja katikati ya vidole vyenu. Lakini Mungu atawahukumu siku moja. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Haikuwa kundi la upuzi, ama mzee fulani mwenye kichaa aliyechochewa sana. Sivyo. Kwa maana, ni Neno la Bwana.

181 Na Mkristo wa kweli na aliye halisi atapata na mtu huyo wa ndani, huyo Roho aliyekuwa kule ng’ambo hapo mwanzo, ambaye ni Neno.

182 Kama vile Yeye alivyokuwa utimilifu wa utu wako wote, ulikuwa katika Yeye kule nyuma katika Kalvari. Yeye alitangulia kujua ya kwamba ungekuwa hapa. Alitangaza tu kitakachotukia. Nawe ulikuwa ndani Yake; ulikufa pamoja Naye. Ulikifia kiburi chako, ukaifia mitindo yako, ukaufia ulimwengu. Wakati Yeye . . . Ulikufa pamoja Naye pale Kalvari, kisha ukafufuka pamoja Naye wakati alipofufuka tena siku ya tatu. [Ndugu Branham aligonga mimbara mara tatu—Mh.] Na kwa sababu wewe umekubali jambo hilo, sasa unaketi katika Ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu. Haleluya!

183 Haya basi. Ni huyo mtu wa ndani. Huyo wa ndani ambaye ataliitikia Neno, atadumu na Neno, haidhuru. Huwezi kujizuia. Nilijifunza jambo hilo, miaka mingi iliyopita.

184 Mtoto wangu mdogo akikaa hapa, anakufa. Mke wangu akilala hapa katika . . . katika—katika chumba cha maiti, amehifadhiwa kwa dawa na kulazwa. Waliniita kule, naye Sharon alikuwa anakufa. Hayo ndiyo majaribio magumu sana niliyopata kukabili maishani mwangu. Nilikuwa na umri wa kama miaka ishirini na mitano. Nikaenda kule nje, naye Billy Paul alikuwa amelala akiwa mahututi.

185 Daktari Sam akaja, kasema, “Bill, sidhani tutamwoko Billy. Nami. . .” Yeye akasema, “Ni mgonjwa sana.” Kasema, “Bill, ninakusikitikia sana.” Akanikumbatia.

Nikasema, "Dakt, sina nguvu zaidi."

¹⁸⁶ Masaa kadha nikimwita mtoto wangu mchanga, Sharon. Nilikimbia kwake kule, yeye...kumwona katika mpindo wa misuli; haungeweza kwisha. Wakamdunga sindano kwenye uti wa mgongo; wakauchoma sindano, wakatoa dokezo, homa ya uti wa mgongo. Hivyo tu.

¹⁸⁷ Nikayumbayumba nikatoka mle hospitalini; nikasimamisha gari langu kuukuu pale nje, nikatoka na kuanza kushuka kwenda kule chumbani. Huyu hapa Sam anashuka kuja kwenye ukumbi, huku ameshika kofia yake mkononi mwake, analia, akanikumbatia, kasema, "Rudi, Bill."

Nikasema, "Kuna nini."

Kasema, "Huwezi kumwona." Kasema, "Yeye anakufa, Bill."

Nami nikasema, "La, Sam, si mtoto wangu."

¹⁸⁸ Kasema, "Naam." Kasema, "Hata usiombe kwa ajili yake, Bill. Kama akiishi kamwe," kasema, "atateseka." Kasema, "Daima angekunjamana, naye angeteseka maishani mwake mwote." Kasema, "Ana homa ya uti wa mgongo." Kasema, "Usiende karibu naye; uta—utamua tu Billy kwa kufanya jambo hilo."

Nikasema, "Sam, sina budi kumwona."

¹⁸⁹ Kasema, "Huwezi kufanya jambo hilo, Bill. Na—nakukataza. Naam, unajua jinsi ninavyokupenda, nawe ni rafiki msiri wangu na kila kitu," akasema, "jinsi ninavyokupenda," kasema, "na jinsi ninavyokuamini, Bill," kasema, "bali usi—usiende kwa yule mtoto mchanga." Kasema, "Kama ukifanya jambo hilo, . . . Homa ya uti wa mgongo imemshika." Mnaona? Kasema, "Yeye ataaga dunia katika dakika chache, na," kasema, "unaweza . . . tutamzika." Kasema, "Bill, kweli ninakusikitikia."

¹⁹⁰ Akamwita—akamwita nesi, kuniagizia namna fulani ya dawa. Kasema, "Sijui jinsi huyu mtu anavyostahimili."

¹⁹¹ Nikasimama pale kidogo. Akaleta ile dawa. Nikaketi chini, kwenye ukumbi. Yeye akasema, "Keti." Naye yule nesi akaileta, kasema, "Kunywa hii, Ndugu Branham."

¹⁹² Nikasema, "Asante. Iweke tu pale kwa muda kidogo." Wakati alipoondoka namna hiyo, nikaimwaga kwenye tasa ile; nikaiweka ile glasi chini tena.

¹⁹³ Nikaketi pale. Nikawaza, "Ee Mungu, nimefanya nini? Wewe ni Mungu mwema. Kwa nini ukamwacha afe, juzijuzi, mimi nikishika mikono yake miwili midogo namna hiyo?" Nikimsihi Yeye kwa ajili yake. "Kwa nini umwache aage dunia? Yule pale Billy amelala, anakufa; naye huyu hapa, anakufa. Nimefanya nini? Niambie! Vema, hata afadhali nami niage dunia pamoja nao."

¹⁹⁴ Nikafungua mlango, na hakuna nesi mwingine aliyekuwa pale. Nikaingia kisiri kwenye chumba cha chini. Hiyo ilikuwa kabla ile hospitali kujengwa. Mapazia, hakuna mapazia madirishani, karibu hakuna, na nzi kwenye macho yake madogo. Alikuwa na kipande cha chandarua cha mbu, tunavyokiita, kilichowekwa juu ya uso wake. Nikawafukuza nzi; amelala pale. Macho yake madogo, alikuwa anaumwa sana hata yalikuwa makengeza.

¹⁹⁵ Ndipo Shetani akasogea karibu nami pale, kisha akasema, “Ati ulisema Yeye alikuwa Mungu mwema?”

Nikasema, “Naam, nilisema hivyo.”

¹⁹⁶ “Ati ulisema alikuwa mponya. Vema, kwa nini baba yako alifia mikononi mwako kule, nawe huku unaomba, naye ni mwenye dhambi, ukiyaombea maisha yake? Kwa nini ndugu yako akafa kwenye mikono ya yule ndugu yako mwingine, kule nje, nawe huku umesimama mimbarani ukihubiri, majuma machache yaliyopita?” Kasema, “Basi kwa nini Yeye hakukujibu? Ulisema Yeye alikupenda na alikuokoa.”

¹⁹⁷ Yeye hangeniambia ya kwamba hakukuwako na Mungu, maana tayari nilikwisha mwona Yeye. Bali alikuwa akiniambia Yeye hakunijali.

¹⁹⁸ Kasema, “Yule pale mke wako amelala. Watoto wako wachanga watakuwa pale hivi karibuni. Baba yako amezikwa. Ndugu yako amezikwa. Naye mke wako atazikwa sasa, kesho. Na huyu hapa yule mtoto wako mwingine mchanga, anakufa. Ati Yeye ni Mungu mwema? En-he? Ati ni mponya?” Kasema, “Ulijipumbaza tu!”

¹⁹⁹ Ilifanya nini? Kutoka... ilikuwa inafanya kazi kutoka upande wa nje, sasa, kwa mtu huyu wa kwanza.

²⁰⁰ Kasema, “Sasa angalia. Unajua, wakati ulipokuwa miaka michache iliyopita, kama miaka miwili au mitatu iliyopita, kabla ya kulikubali Hili, ulikuwa una sifa njema miongoni mwa watu. Uliishi maisha mazuri na masafi. Msichana ye yote mjini, aliyetaka kwenda kutembea, aliambatane nawe, kwa sababu wao walijisikia u msafi na mwadilifu.” Niliweza kusimama mbele ya ye yote wao. Sikumtukana kamwe hata mmoja wao, sikusema kitu. Kama angalijifanya mjuvi, ningempeleka nyumbani. “Nawe ulipendwa miongoni mwa watu. Lakini sasa wewe u nani? Mshupavu wa dini.”

²⁰¹ “Hiyo ni kweli. Nilikuwa hivyo.” Mnaona haya mambo yanaanza kwenda pamoja? Yule wa nje, kuhoji katika roho, akiyaendesha mambo haya pamoja. “Hiyo ni kweli, Shetani.”

“Ati ulisema alikuwa mponya?”

“Naam. Ndiyo.”

²⁰² “Nawe huku unaomba dua na kulia, na hao watu wakikwambia haikuwa hivyo, ya kwamba umetoka kabisa

kwenye njia. Kanisa lako mwenyewe lilikufukuza, kwa ajili ya Hili. Kanisa lako mwenyewe la Kibatisti kule chini, lilikufukuza, kwa sababu ile ile.”

“Naam.”

203 “Baba yako amezikwa. Ndugu yako amezikwa. Mke wako amelala pale, atazikwa. Huyu hapa mtoto wako, kama dakika kumi na tano tu zaidi na atakuwa ameaga dunia. Naye ati ni mponya? Ukoo wako mwenyewe; neno moja kutoka Kwake lingeyaokoa maisha ya mtoto huyo mchanga. ‘Yeye ni mponya,’ ulisema. Watu walijaribu kukwambia. Mhubiri alikwambia ya kwamba umechanganyikiwa kabisa; ulikuwa na kichaa; ulikuwa umekuwa shupavu wa dini. Nawe ulisema eti alikupenda. Hivi angeweza kukupenda?

204 “Na jinsi ulivyolia kwa ajili ya baba yako! Jinsi, usiku baada ya usiku, ulifunga, na wakati wewe...mchana, wakati ingekulazimu kuomba, kupanda mti, kufanya kazi. Na huku Yeye alimfanya afie mikononi mwako, mwenye dhambi.

205 “Jinsi mke wako, jinsi alivyokuwa mwanamke mzuri, na jinsi ulivyompenda!” Mama Billy; wengi wenu mnamkumbuka Hope. “Jinsi alivyokuwa msichana mzuri! Jinsi mlivyokuwa na furaha, nyumba yenu ndogo pale; yenye fanicha zenye dhamani ya dola saba ama nane, fanicha mlizokuwa nazo, bali hata hivyo ulimpenda; nawe...nanyi mlipendana. Nawe uliondoka ukaenda ukawaombea wengine; na, msisimko fulani wa akili, wakaondoka wakaenda wakasema walikuwa wamepona. Lakini sasa mke wako mwenyewe; naye huyo hapo, amekufa, siku ya pili sasa, amelala katika chumba cha maiti kule, Scott and Combs. Ati ni mponya? En-he?

206 “Na mvulana wako akiwa mahututi, Billy Paul, mwenye umri wa miezi kumi na minane. Na msichana wako mchanga, mwenye umri wa miezi minane, amelala hapa, yuafa, kwa homa ya uti wa mgongo. Nawe ndiyo kwanza uombe; kisha Mungu akashusha shuka, kasema, ‘Nyamaza! Sitaki kusikia, sitakusikia, hata kidogo!’ Akakupa kisogo. Ati Yeye ni Mungu mwema? En-he? Ati anakupenda? Na kila msichana uliyewahi kuandamana naye, kila mvulana uliyewahi kuhusiana naye, marafiki wako walio wazuri sana, wamekuacha kama shupavu wa dini.”

207 Kila kitu alichokuwa akiniambia kilikuwa ni kweli. Kila kitu ambacho yeye angesema, kiliingia tu mstarini, mnaona, hapa. Basi nilikuwa tu karibu tayari kusema, “Basi mimi, kama hivyo ndivyo inavyombidi Yeye kutenda, basi mimi sitamtumikia.”

208 Mara niliposema hayo, kulikuwa na Kitu kilichokuja kutoka mahali pengine, kule chini kabisa kwa ndani. Kasema, “Wewe ni nani ati, kwanza? Bwana alitoa, na Bwana ametwaa.” Mwaona, huyo ni huyo mtu wa ndani, hahoji hata kidogo.

209 Nikaangalia nyuma, nami nikawaza, “Nilikujaje duniani? Nilitoka kwenye kundi la walevi. Nilikujaje hapa? Ni nani aliyenipa uhai? Ni nani aliyenipa mke yule? Ni nani aliyenipa yule mtoto mchanga? Mke wangu alitoka wapi? Uhai wangu ulitoka wapi?” Nikasema, “Hata Yeye akiniva, hata hivyo nitamtumaini.”

Nikasema, “Ondoka kwangu, Shetani!”

210 Nikaiweka mikono yangu juu ya huyo mtoto mchanga. Nikasema, “Sharon, kipenzi, nitakuweka kwenye mikono ya mama yako katika dakika chache, wakati Malaika wa Mungu atakapokuja kukuchukua, lakini siku moja baba atakuona tena. Sijui itakavyokuwa, kipenzi. Siwezi kukwambia ni namna gani; wakati Yeye anaponipa kisogo, hata hatayasikia maombi yangu kwa ajili yako.”

211 Yeye alimwacha mke wangu afe, nami huku nimemshika kwa mikono, nikilia kwa ajili yake. Na baba yangu, mikononi mwake, alikufa juu ya mkono huu papa *hapa*; akiniangalia, akijaribu kupumua. Nami niliomba kwa bidii sana nilivyoweza. Ningaliwezaje kuwakabili watu tena, kuhubiri juu ya kuponya Kiungu? Ningewezaje kuhubiri ya kwamba Yeye alikuwa Mungu mwema, halafu anamwacha baba yangu mwenyewe afe, mwenye dhambi? Ningewezaje kulihubiri jambo hilo? Sijui ni vipi, bali najua ya kwamba Yeye yu sahihi.

212 Neno la Mungu halitashindwa kamwe. Litashinda, hata iwe nini. Ndipo nikajua kuna Kitu fulani ndani ya hoja zote, Kitu fulani ndani ya misisimko yote, kila kitu kingine namna hiyo. Kulikuwa na mtu wa ndani, na huyo alishikilia katika saa hiyo. Hakuna kitu kingine kingeweza kufanya jambo hilo; kila hoja, kila kitu kingaliweza kuonyeshwa, kila kitu kingalithibitisha kwamba Hilo lilikuwa ni kosa, nami nilikuwa makosani. Lakini Neno la Mungu, ambalo lilikusudiwa tangu zamani kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, lilishikilia mle ndani.

213 Nikasikia Upepo mdogo ukipitia mle chumbani. Roho yake ikaenda kukutana na Mungu.

214 Ndugu, dada, hebu nikwambie, Hicho ndicho kitu pekee. Usijaribu kulihoji Hilo. Usijaribu kuwa na nywele ndefu ati kwa sababu nilisema hivyo. Usijaribu kufanya mambo haya kwa sababu tu, kwa sababu, katika mwili wako. Usijaribu kufanya jambo hilo, kuchukuana tu kwa namna fulani. Bali ngojea tu mbele za Bwana, hata Kitu fulani kule ndani kabisa!

215 Wengi wenu mnafikiri, kwa kuwa mna nywele ndefu, hiyo ina maana ya kwamba mtaenda Mbinguni. Hiyo haimaanishi hivyo. Wengi wao hufikiri, kwa kuwa wewe ni mwanamke mzuri, mwadilifu, uaenda . . . ? . . . Haimaanishi hivyo. Wengi wao wanafikiri, kwa kuwa makanisa yao, nao ni wafuasi wa *hili*, na makundi *haya* makubwa, na madaktari wakuu wa Ungu. Hilo halimaanishi hivyo. Mnaona?

²¹⁶ Wengi wanafikiri, kwa kuwa wananena kwa lugha, wana Roho Mtakatifu. Hilo halimaanishi hivyo. Ingawa, Roho Mtakatifu kweli hunena kwa lugha. Lakini mpaka huyo Roho Mtakatifu halisi na wa kweli mle ndani atakapopatana na kila Neno! Kama huyo Roho Mtakatifu aliye ndani yako, ambaye anakufanya kunena kwa lugha; anaangalia kule nyuma na hakubaliani na Neno lingine lote, basi ni roho mbaya. Mnaona?

²¹⁷ Haina budi kuja kutoka ndani, ambalo ni Neno, tangu mwanzo. “Katika mwanzo wa kuumba kwa Mungu,” wakati Mungu alipoanza kuumba, akikufanya uishi, unaona. Ulianza kule nyuma kama mbegu, na ukaendelea hadi mahali ulipo sasa. Ndipo, basi, nyote mlikuwa katika Kristo. Halafu wakati Kristo alipokufa, Yeye alikufa kusudi awakomboa ninyi nyote. Nanyi ni sehemu ya Neno *hili*, basi mnawezaje. . . Biblia, Yote! “Amri juu ya amri, kanuni juu ya kanuni; huku kidogo, na huku kidogo.” “Hakuna yodi moja ama nukta moja itakayoshindwa.” Unawezaje kamwe, ukiwa sehemu ya Neno hilo, kutokubaliana na lingine lote, ama sehemu yo yote Yake?

²¹⁸ Mungu awabariki. Nimepita wakati sasa. Sikumaanisha kufanya jambo hili, kuwaweka kwa muda mrefu hivi. Samahani kwa maana niliwaweka; si samahani kwa yale niliyosema.

Tuko kwenye mwisho kabisa wa kitu fulani, enyi marafiki.

²¹⁹ Nanyi nyote hapa, nafikiri, ni washiriki tu wa hapa wa kanisani. Mimi siji hapa, kwa wakati ufao, kuona ni washiriki gani waliopo. Nadhani ninyi nyote mnakuja hapa kila wakati. Hebu niwaambieni jambo fulani lililotukia. Mtanipa, tuseme, dakika sita zaidi? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

²²⁰ Kasisi Bw. O. Walker hapa kutoka Oregon, ambaye alikuwa hapa Jumapili ile—ile niliyokuwa hapa? Kuna mtu anayejua jambo hilo? Lilikuwa jambo kubwa na la ajabu.

²²¹ Nilishuka nikaja hapa, kulikuweko na watu wengi sana ndani, ni—nilikuwa. . . nilikuwa na rundo la mahojiano, na kila moja ya hayo yalikuwa muhimu; mvulana wao, watoto, walioolewa, walevi, na—na mambo mbalimbali, na mambo tu yaliyokuwa muhimu. Kila mmoja wao alipaswa kuonwa. Siwezi kufanya mambo hayo yote. Nami nawakabidhi kwa Mungu, na kuweka mikono yangu juu yao, katika maombi. Nikasema, “Ee Mungu, ni—nisingeweza kufanya jambo hilo. Wafikie, Bwana, fanya. . . Wewe unajua namna ya kulifanya. Namwombea kila mmoja.”

²²² Billy aliniita. Nami ndiyo kwanza nije na Ndugu Banks. Akasema, “Baba, kama wewe. . .”

²²³ Basi, hebu, angalia, nawaona watu wakiendesha magari kule wakati mwingine, kwenye barabara ndogo, wanaangalia ndani. Nami nawaangalia, kisha nawapungia mkono namna *hiyo*, nao—nao karibu wageuze vichwa vyao. Siwataki mfanye hivyo.

224 Juzi wakati walipokuwa wanapanunua mahali pale kule Tucson nipate kuisha kule. Ndugu Tony alikuwa na mahali kule alipotaka kuninunulia, kwa yapata mara tatu au nne ya bei ya mahali hapa. Hata alitaka kutoa dola elfu kadha kwake, yeye mwenyewe. Bali njia pekee unayoweza kufika pale, mlinzi wa mlango alikuwa amesimama pale. Mtu mkubwa mno. . . Vema, ni nyongeza kule. Lakini ye yote. . . Watu hawa wanaoishi kule, huna budi kuwa na barua ya kukuruhusu, ndipo huyu mlinzi wa mlango anakuita kuona kama ni sawa kwao kuingia.

225 Nikasema, “Ungeweza kuwazia, mimi, ndugu zangu na dada zangu wanaokuja kuniona, ambao wanataka kunipa mkono na kuniombea baraka za Mungu, ungeweza kuniwazia mimi nikijiweka mwenyewe ndani pale, Tony?”

Akasema, “Vema, wewe una- . . .”

226 Nikasema, “Tony, vile kanisa na hao wote wanavyowakataza watu wasije karibu,” nikasema, “hiyo ni kwa ajili ya watu ambao walio na yote wanayotaka mimi kufanya.”

227 Wao, wanasema, “Vema, Bwana aliniambia. Haleluiya! Mimi nitakaa papa hapa. Mungu atukuzwe! Bwana aliniambia huna budi kufanya mkutano hapa kwenye kundi letu. Naam, bwana, Mungu atukuzwe! Mungu aliniambia jambo hilo. Kama hutafanya jambo hilo, Ndugu Branham, kweli umerudi nyuma.” Mimi kule ndani nikijaribu kujifunza, mnaona. Hiyo ndiyo sababu, mnaona. Na watu wengi wazuri wanashindwa, kuja, kwa sababu ya jambo hilo.

228 Ni kama tu mtu akienda kuwinda nje hapa shambani. Mkulima anasema, “Karibu. Unaweza kuwinda.” Nawe unaingia kule na kumpiga risasi mmoja wa ng’ombe zake; sungura alikimbia chini ya huyo ng’ombe, nawe ukamtupia risasi huyo sungura, haidhuru. Unapanda kwenye ua, badala ya kwenda kwenye lango ukapanda kama muungwana anavyopaswa kufanya; unapanda ua na unauvunja namna hiyo. Mnaona? Ndipo yeye atasema, “Nitapafunga mahali hapa!” Si—simlaumu hata kidogo, hata kidogo. Vema, anafanya nini? Yeye anawazuia wawindaji walio waungwana kuja. Ndivyo ilivyo daima. Walio waovu ndio wanaowazuia walio wazuri kuwa na sifa nzuri. Kila wakati.

229 Naam, lakini hao watu ni, maelfu yao kweli ni wahitaji na watu wazuri, watu wa kupendana, wamejaa neema ya Mungu.

230 Sasa tuna jambo hili, vile watu hawa waliingia namna hiyo. Hatutaki, hatutaki jambo hilo, la.

Bali mtu huyu alikuja. . .

231 Billy alisema, “Shuka uende mbio, haraka sana, baba.” Kasema, “Bibi Waldorf yuko chini hapa na watu wanaokufa; hana budi kuwaona mara moja.” Nami nikakimbia kule; nikashuka nikaja hapa.

²³² Na niliporudi, wao walisema, “Hakuna mtu hapa chini isipokuwa mtu mmoja anayelala katika upande wa upande, kule nje, kwenye mto kila siku, kando ya hili jengo.” Kasema, “Yeye anakutaka umwombee.”

Nikasema, “Sawa.” Kasema, “Nitamweka ndani.” Nikaingia.

²³³ Kulikuwa, nafikiri, na Kadilaki imewekwa hapa nyuma upande wa nyuma, ama namna fulani ya motokaa kubwa. Nikaja, nilikuwa. . . Ndipo huyo mtu akasema, “U hali gani.” Yeye hakunijua.

²³⁴ Basi nikaingia. Naye Dada Waldorf, maskini mtu huyo, akaingia. Mwajua, yeye alikuwa. . .

²³⁵ Mnajua kisa chake, sivyo? Mnaona, yeye alikuwa na kansa; akafa kwenye mstari wa maombi, kama saa moja kabla sijamfikia. Daktari wake akaja, akanionyesha. . . Hiyo imekuwa kama miaka kumi na minane iliyopita, kansa moyoni, mnaona, naye anaishi leo. Naye anaishi kule Arkansas sasa.

²³⁶ Naye alikuwa kule Phoenix, wakati huo. Ndipo akasema, “Ndugu Willie, nilichukia kuingia namna hii, lakini,” kasema, “sikuwa na mahali pa kukaa. Nilichukia. . . Walisema watu hawa, mwanamke huyu atakufa, Ndugu Willie.”

²³⁷ Kasema, “Nilitaka kukuletea sadaka ndogo mkononi mwangu, Ndugu Willie,” kasema, “lakini nisingeweza kufanya jambo hilo. Ila nilitia koponi siagi ya forosadi.”

²³⁸ Loo, nilipokwenda kule na kuona hizo glasi ndogo za siagi alizokuwa nazo zimewekwa pale, mimi. . . zilionekana takatifu sana kwangu kuzila. Mnaona? Mwanamke huyo mzee mpendwa, aliye na kama umri wa miaka sabini. Nikasema, “Dada Hattie. . .” Ni—nisingesema la. La. Yesu alimwona yule mjane akitoa peni tatu, Naye ha—ha—hakumzuia. Mnaona? La. Mungu atamjazi kwa jambo hilo. Naam.

²³⁹ Na kwa hiyo Bwana akamponya huyo mwanamke, akawaponya wale wote aliokuwa nao, akamfunulia mchungaji wake yale yeye, mwanamke, alikuwa nayo moyoni mwake, kile mchungaji anapaswa kufanya, jambo jingine. Na, loo, wote wakatoka, wakipaza sauti.

²⁴⁰ Ndipo Billy akaingia mbio. Akasema, “Baba, mtu huyo ameondoka. Siwezi. . .”

Nikasema, “Ni nani yule kule nje kwenye motokaa?”

²⁴¹ “Loo,” yeye akasema, “jamaa fulani aliyetoka Oregon, alisema ana ndoto ya namna fulani. Nami nikamwambia, ‘Siwezi kukupa tumaini lo lote la uongo. Kuna mia tatu hapa, wanaongoja sasa.’ Kisha kasema, ‘Nami nikamwambia, ‘Andika tu hiyo ndoto.’ Kasema, ‘Nina rundo lazo hapa, kubwa hivi, hata hivyo, nami nitaiongezea tu kwazo.’”

Nikasema, “Mlete ndani. Mpe dakika tano.”

²⁴² Vema, mara yule mtu alipoingia; dakika tano? Yeye akasema, “Mimi ni Kasisi Walker,” nafikiri jina lake lilikuwa hilo, “kutoka Oregon.” Nafikiri ni wa madhehebu fulani, sijui, Mpresbiteri, Mpresbiteri fulani.

²⁴³ Akasema, “Nilikutana nawe yapata miaka ishirini iliyopita. Nilishuka nikaja kule Grants Pass ambako wewe. . .” Ama, si Grants Pass, bali nilisahau jina la mahali pale. “Pale,” kasema, “nchi nzima, vichwa vya maneno magazetini kila asubuhi.” Kasema, “Kila mtu alijua jambo hilo.” Kasema, “Hata nisingeweza hata kuingia kwenye lile jengo ulilokuwemo, bali nilikuona ukipanda kwenda kule. Basi siku moja, barabarani, nilipanda nikaja,” kasema, “watu wanne watano wamekuzunguka, kisha nikakupa mkono. Nawe. . . Nilikwambia nilikuwa Ndugu Walker, nawe ukaniambia ulikuwa nani.” Kasema, “Tulizungumza maneno machache, kisha watu watatu wanne wanene uliokuwa nao wakakusukuma mbele.” Akasema, “Mimi sikuwa ninakulaumu, wala sikuwa upande wako.” Yeye akasema, “Ni kwamba tu mimi sikufahamu.”

²⁴⁴ Akasema, “Iliendelea namna hiyo kwa miaka michache, na baada ya kitambo kidogo,” kasema, “mimi. . . mtu fulani akaniambia niye nisikize kanda fulani, yapata miaka mitatu iliyopita.” Kisha kasema, “Mtu huyo alicheza hizo kanda. Ndipo, alipofanya hivyo,” akasema, “nikamsikia akizungumza.” Kisha akasema, “Mtu huyu aliamini ya kwamba wewe ulikuwa na—nabii. Nikasema, nikamwambia mtu huyo, ‘Sijui juu ya mambo hayo; huenda ikawa, nijuavyo mimi.’”

²⁴⁵ Kwa hiyo, kasema, “Kisha mtu mwingine akahamia kwenye mji wetu, akafanya mkutano, nami nikakutana naye. Ndipo akasema, ‘Mimi ndimi nabii wa Mungu wa siku hii.’”

²⁴⁶ Yeye akasema, “Ninyi mu jamaa wangapi hata hivyo? Kasema, ‘Na—na—nasikia ambapo mtu mmoja huku chini anasikiza kanda, kasema, “William Branham, kule nyuma mashariki, alikuwa nabii wa siku hii,” na mambo kama hayo.”

²⁴⁷ Akasema, “Mtu huyu. . .” Sitalitaja jina lake, maana haisikiki sawa, hapa, manaona. “Naye akasema, ‘Najua William Branham,’ kasema, ‘lakini yeye amekosea kabisa katika Fundisho lake.’ Kasema, ‘Yeye si Mpentekoste; yeye haamini katika ushuhuda wa kwanza.’ Kisha akasema, ‘Jambo jingine, yeye anasema kuna manabii wakubwa na wadogo. Hakuna kitu kama hicho.’ Kasema, ‘Wewe ni nabii ama wewe si nabii, na ni hilo tu.’”

²⁴⁸ Akasema, “Vema, bwana, mimi. . . sikubishana nawe juu ya jambo hilo. Nilisema tu nilimsikia mtu huyu akisema ya kwamba mtu huyu, William Branham. . . na ya kwamba mtu huyu alidai kuwa nabii.” Kasema, “Sikujua ua tu walikuwepo wangapi.”

249 “Akasema, ‘Bali nawataka mjue jambo hili. Mimi ndiye nabii wa wakati huu.”

250 Akasema, “Vema, ndiwe?” Kasema, “Bwana akubariki na awe pamoja nawe.”

251 Akaendelea, hakulijali jambo hilo. Kisha akasema akaanza, miongoni mwa ndugu zake, mfululizo wa mikutano mitatu minne. Naye akashuka akaenda kwenye posta, kasema, “Usi—usibadilishe barua zangu. Ziache hapa mpaka nitakaporudi, kama siku nne ama tano baadaye.”

252 “Sawa,” wao wakasema. Wakaweka tikiti pale, zisibadilishwe.

Akashuka akaenda akamwona binti yake.

253 Na alipokuwa anaenda zake barabarani, a—akasimama kwenye kanisa fulani. Naye alihubiri mkutano wa usiku ule. Asubuhi iliyofuata, alisema ilitukia tu kwamba aliwaza, “Nenda ukazichukue barua.” Na alipofanya hivyo, barua moja ilikuwa imejipenyeza kwenye posta ikamfikia binti yake; binti yake akaituma kule, kama barua ya kawaida.

254 Naye akaifungua. Akasema ilikuwa mwanamume. Bw. Hildebrandt, ambaye ni rafiki yangu, ambaye alikuwa yule mtu aliyekuwa anacheza kanda. Kasema Bw. Hildebrandt alikuwa amezungumza na Roy Borders (na huyo ni mmoja wa mameneja, mwajua), ya kwamba nilikuwa naenda kufanya mkutano hapa, kutoka tarehe ishirini na nane hadi tarehe moja, nije nijionee mwenyewe.

255 Yeye akasema, “Sasa, angalia hapa, jamaa hao wanajaribu kunivuta kwenye kitu kama hicho!” Mnaona? Ndipo akaitupa ile barua kwenye kikapu cha takataka, halafu akaendelea mbele, mnaona, namna hiyo. Akaenda na kufanya mkutano huo usiku huo. Ndipo asubuhi iliyofuata . . .

256 Ndipo akaanza kuushikilia moyo wake, kulia, papo hapo chumbani.

257 Akasema, “Bw. Branham, ninatambua sina budi kusimama mbele za Mungu.” Akasema, “Sijui kama nilikuwa nimelala ama nini kilichotukia.” Akasema, “Niliota. Nitasema nilikuwa nimelala kisha nikaota.”

258 Kasema, “Niliwaza mwanangu, sokoni, alitumbukiza mkono wake katika gu—gunia.” Kisha kasema, “Alipofanya hivyo, lilikuwa gunia la matofaa, nayo yote yakaanguka.” Kasema, “Nilipoenda kuyaokota, yote yalikuwa matofaa mabichi yaliyokuwa yameumwa mara moja.” Kasema, “Nilikuwa nikiyaokota, nikayarudisha kwenye lile gunia.” Kasema, “Mengine yao yalifingirika yakatoka, yakafingirika sakafuni, kwa hiyo nikaenda kujaribu kuyachukua, na chini . . . kwenye nyasi.” Kisha akasema, “Yalifingirika chini ya moja ya hizi nyua za nyororo za vifuli. Na kulikuwa na barabara kubwa sana

iliyoenda kule. Nikaangalia nyuma mashariki, na,” akasema, “ile—ile—ile nyororo ilifungiliwa kwenye mwa—mwamba mkubwa kule nyuma mashariki. Ndipo nikarudi kule, nikafikiri ningeweza kuishusha chini nyororo hii, kisha niende kule na nikamchukulie yule mtu yale matofaa.” Kasema, “Nikaanza kuishusha ile nyororo.”

²⁵⁹ Kasema, “Sauti ikaitisa dunia nzima.” Kasema, “Dunia ikatetemeka, chini ya miguu yangu.” Akasema, “Ilipoacha kutetemeka, nikasikia sauti.” Ndipo akasema, “Ndugu Branham, ilikuwa ni sauti yako,” kasema, “nilijua; kuna kitu fulani kilichosema hivyo.” Kasema, “Ilisema, Nitapanda farasi kupitia njia hii tena!”

²⁶⁰ Kisha akasema, “Nikaanza kuangalia juu ya ule mwamba, namna *hii*, na nikazidi kuangalia, kupita mawingu. Na kule juu kabisa, nikisimama kwenye mwamba uliotandaa kutoka mashariki kwenda magharibi, katika umbo lililochongoka namna *hiyo*, kama piramidi, ukatandaa nyuma hapa kuelekea mashariki, na,” kasema, “pale ulikuwa umesimama pale, juu ya farasi ambaye sijawahi kuona kitu kingine kama yeye maishani mwangu mwote; farasi mkubwa sana mweupe, huku manyoya ya shingoni yamening’inia chini.” Kisha kasema, “Ulikuwa umevalia kama chifu wa Kihindi, ukiwa na vitu vyote ambavyo Wahindi hutumia.” Kasema, “Alikuwa na dirii; hivyo vikuku mikononi, na kote chini namna *hiyo*.” Kasema, “Ulikuwa umeinua mikono yako namna *hiyo*.” Kisha kasema, “Huyo farasi amesimama pale kama farasi wa kijeshi, akichezacheza namna *hii*, akitembea,” huku mimi nimesimama kimya. Ndipo nikasema, “Ulivuta hatamu, akaenda shoti kuelekea magharibi.”

²⁶¹ Kasema, “Niliangalia kule chini, na kulikuwa na wanasayansi wengi sana.” Na asubuhi iliyofuata...Hiyo ilikuwa Jumamosi. Asubuhi iliyofuata, nilihubiri juu ya wanasayansi, mwajua, kuwa ni wa ibilisi. Kisha nikasema, “Wanasayansi pale walikuwa wakimwaga vitu kwenye tyubu, na kuvichanganya.” Kasema, “Ukasimamisha farasi, ukainua mikono yako tena na kupaza sauti, Nitapanda farasi kupitia njia hii tena!” Kisha kasema, “Dunia nzima ikatetemeka. Hao watu wakatetemeka,” kasema, “wakainua macho yao kisha wakaangaliana, namna *hiyo*, kisha wakainua macho yao wakakuangalia. Wakakunja mabega yao tu, wakaendelea na utafiti wao wa kisanyansi.” Ndipo kasema, “Wewe ukaanza kwenda kuelekea magharibi.

²⁶² “Na wakati ilipofanya hivyo,” kasema, “nikamwona mtu huyu aliyekiita nabii, mwajua,” kasema, “alikuja amepanda farasi iliyokuwa mchanganyiko wa rangi nyeupe na nyeusi pamoja.” Ndipo akasema, “Yeye alisogea akaja nyuma ya huyu farasi mkubwa mno.” Kasema, “Ilikuwa,” kasema, “kule juu kabisa juu ya mawingu, na ile barabara haikuwa pana *hivi*.”

Ndipo akasema, “Huyo farasi alininino tu. . .” Kasema, “Upepo ukipeperusha manyoya na kila kitu kwe—kwenye mavazi yako,” kisha kasema, “halafu manyoya ya shingoni ya huyo farasi na mkia yakipeperushwa. Farasi hodari sana, mkubwa na mweupe, akitembea moja kwa moja mstarini.” Ndipo akasema—akasema, “Jamaa huyu akaenda shoti nyuma yako, akitoka upande wa Canada,” na mtu huyo anaishi Canada. Naye akasema, “Akarudi, na,” kasema, “akamchukua farasi wake mdogo, akijaribu kumwangusha farasi wako; akimgeuza; akafanya viweo vyake vigonge ninino. . .” Kasema, “Haikumsogeza huyo farasi mkubwa; yeye aliendelea tu kutembea.”

²⁶³ Kasema, “Kisha, mara,” kasema, “ukageuka.” Kasema, “Hiyo ingekuwa mara ya tatu ulikuwa umezungumza, bali mara ya pili uliposema Nitapanda farasi.” Ndipo kasema, “Hukuzungumza kama ulivyofanya. Uliamrisha.” Kasema, “Uligeuka kisha ukamwita yule mtu kwa jina lake, kasema, ‘Ondoka hapa! Unajua ya kwamba hakuna mtu anayeweza kupitia kwenye barabara hii hapa bila ya Mungu kumwagiza kufanya hivyo. Ondoka hapa!’”

²⁶⁴ Kisha kasema, “Yule mtu akageuka.” Kisha kasema, “Mtu huyu ameniandikia barua.” Ndipo kasema, “Kwenye viweo vya farasi wake,” huyo mweusi na wa kijivujivu, zilizochanganyikana, kasema, “kwenye viweo vya farasi wake liliandikwa jina lake, sahihi kama ile hasa iliyo kwenye barua zake. Naye akaelekea kaskazini.”

²⁶⁵ Kasema, “Kisha ukashuka ukaenda; huyo farasi mkubwa akageuka, huko mbali magharibi ulivyoweza.” Kasema, “Ulisimama na kuinua mikono yako juu namna *hiyo*. Ndipo akaanza kulia. Kasema, “Ndugu Branham, kumwona huyo farasi amesimama hapo; kofia hiyo yote ya vita na kila kitu namna hiyo, na,” kasema, “hiyo dirii ya kifuani na kila kitu kinametameta.” Kasema, “Uliinua mikono yako juu kwa muda kidogo.” Kisha kasema, “Uliangalia chini tena, ukachukua hatamu, kasema, ‘Nitapanda farasi kupitia njia hii tena!’” Kasema, “Dunia nzima ikatetemeka huku na huko, namna *hiyo*.” Kisha kasema, “Hapakuwepo na uhai ulioachwa ndani yangu tena; nilianguka tu chini kando ya ule mwamba. Kisha nikaamka.”

Kasema, “Hiyo ina maana gani, bwana?”

Nikasema, “Sijui.”

²⁶⁶ Asubuhi yake. . . Junior Jackson, aliyeota juu ya piramidi, mwajua, nilipoenda magharibi. Mnakumbuka jambo hilo. Yeye alinipigia simu, mwezi mmoja ama miwili kabla ya jambo hilo. Alikuwa na ndoto iliyokuwa ikimwasha; ilimbidi kuniambia. Nami nikasema, “Billy. . .”

²⁶⁷ Kulikuweko na yapata ishirini waliokuwa wamesimama pale. Akasema, “Junior Jackson, kule chini, alisema ilimbidi akwambie ndoto hiyo.”

Nikasema, “Mwingize ndani, kwa kama tu dakika tano.”

²⁶⁸ Akamleta mke wake, na, akasema, kama shahidi. Akasema, “Niliota ndoto, Ndugu Branham, mimi na mke wangu tulikuwa huko nje tukipanda farasi. Nami nikasema, “Niliangalia nyuma upande wa mashariki, nami nikaona, ilionekana kama, kitu kidogo, moja ya hivyo visahani virukavyo.”

²⁶⁹ Mnaona, ulimwengu haujui hivyo ni nini, mwajua. Mnajua viko. Tunajua hivyo ni kitu gani. Mnaona? Tunajua ni Malaika wanaochunguza, wa hukumu, mwaona. Na jinsi huwa kule kwenye Ikulu na kadhalika, jinsi kinavyoshuka moja kwa moja chini; na hizo akili, jinsi wanavyoweza [Ndugu Branham anadata vidole vyake mara moja—Mh.] wanaondoka kama umeme na kutoweka, wanaondoka kwenye kila kitu walicho nacho. Mnaona, wao hawatambui ni nini, mnaona. Acheni wafikirie cho chote watakacho. Wao wanaita visahani virukavyo, ama cho chote kile. Hawajui, mnaona.

²⁷⁰ Kasema, “Nami nikakiona kikija, nami nikakiangalia. Na jambo lilikuwa ni kwamba, ilikuwa ni mtu fulani amepanda farasi.” Kisha kasema, “Yeye alikuwa anakuja kwa mwendo wa umeme.” Kasema, “Niliona alikuwa anashuka mbele yangu. Ndipo nikasimamisha motokaa yangu, nikaruka nje. Nilipofanya hivyo,” kasema, “motokaa...farasi alikuwa amesimama barabarani, farasi mkubwa sana mweupe wa kijeshi akichezacheza.” Hilo ni Neno, bila shaka, mwajua, likitembea likichezacheza.

²⁷¹ Kasema, “Kulikuwa na mtu aliyekuwa ameketi hapo juu.” Kasema, “Yeye—yeye alikuwa amevaa mavazi ya kimagharibi; hakuwa cowboy, lakini,” kasema, “alionekana kama chifu anayewaongoza wasimamizi wa mwitu ama cho chote kile.” Mnaona, mamlaka yote yake ya chifu, kutoka magharibi; Wahindi juu ya Wahindi; wasimamizi wa mwitu juu, mnaona. Kisha kasema, “Yule mtu alikuwa ameivuta kofia yake chini, na alikuwa...alikuwa akiangalia kando.” Kisha akasema, “Wakati alipoangalia kando,” kasema, “ilikuwa ni wewe, Ndugu Branham.” Kasema, “Hukuzungumza kama ulivyofanya. Ulisema, ‘Junior!’ Kamwita mara tatu. Kisha kasema, ‘Nitakwambia la kufanya’ Ndipo kasema, “Ndipo ukavuta hatamu za huyu farasi. Uliiruka kama mara tatu, ndipo ukaingia angani, nawe ulikuwa umeenda kuelekea magharibi.”

²⁷² Yeye akasema, “Hebu kidogo, nikaangalia kila mahali, halafu akaja farasi mdogo kuliko huyo, wa ukoo ule ule, lakini ni mdogo, kisha akasimama.” Kasema, “Nikatembea kila mahali, kasema, ‘Hapana budi alimtuma huyu kwa ajili yangu.’ Kasema, “Nikampanda.” (Junior amepanda

farasi kidogo, pia. Akasema, “Unajua jinsi matandiko yako yanavyokukaa Ndugu Branham, vikuku na kadhalika?” Kasema, “Nilifikiri, vema, haya yananikaa vizuri sana. Kwa hiyo nikavuta hatamu, nikaruka hewani.” Kasema, “Nilivuta hatamu nikamsimamisha, nikageuka nikarudi. Mnaona? Niliporudi,” kasema, “nilimsimamisha huyo farasi, nikatoka na kuzungumza na mke wangu. Yule farasi akaondoka.” Naye akasumbuka sana.

²⁷³ Halafu, juzijuzi, siku tatu zilizopita, akaja Leo Marcier, akashuka akaja na ndoto ile ile hasa, bila kujua jambo lo lote juu yake; juu ya kujaribu kumzalisha farasi dume mkubwa mweupe na farasi jike mweusi, nao hawangeweza kufanya jambo hilo; wasiwasi. Kasema nilipanda nikaenda kule, kasema, “Leo,” na kumwambia nilichomwambia. Sitaki kusema jambo hilo hapa, mnaona, bali nilimwambia niliyomwambia. “Kasema, ‘Je! huoni? Sasa, kujua jambo hili; sikumjua Ed Dalton alikuwa na mwana mkwe, naye huyo mwana mkwe alikuwa na mbwa mwenye jina hili. Utajua, Leo, ya kwamba unaota. Lakini, unapoamka, ikumbuke!’” Kisha akasema, “Sijasikia kamwe amri kama hiyo.”

²⁷⁴ Yapata wakati huo, Roy Roberson akaingia, kasema, “Ndugu Branham, unakumbuka kule nyuma kabla hujaondoka kanisani mara ya kwanza? Tulikuwa... Nilikuona umeketi, kama kwamba ni katika Palestina. Sisi sote, halmashauri na kila kitu, tulikuwa tumeketi kana kwamba ni meza ya Bwana, kisha ukazungumza. Nawe... Yeye hakuwa na uhakika na yale uliyokuwa unazungumzia.” Kasema, “Wingu jeupe lilikuja likakuchukua, likakubeba.” Ni wangapi wanakumbuka ile—ile ndoto ya Ndugu Roy? Kisha kasema, “Lile wingu jeupe lilikuchukua,” kisha kasema, “ndipo ukatoweka. Nikatembea barabarani, nikipiga kelele na kulia.”

²⁷⁵ Nilipokuja hapa nje, na maskini huo mkono wa kale umelemaa, kama alivyokuwa, akisoma hili. Aliangusha jembe la meno na akaanza kulia aliponioana nikija kule nje. Sikua nimemwona kusudi aniambie hiyo ndoto. Naye akasema... Naye alikuwa anatomia jembe la meno. Nikasema...

²⁷⁶ “Na—nawe ukaondoka ukaenda.” Kasema, “Nilitembea barabarani, kila mahali, nikijaribu kukutafuta. Singeweza kukupata, mahali po pote. Nilikuwa nikipaza sauti, ‘Loo, Ndugu Branham, usiondoke!’” Kasema, “Wingu jeupe lilikuja likakuchukua, likakuondoa kwetu, likakupeleka upande wa magharibi.” Hiyo ilikuwa kabla ya ile Piramidi ama cho chote kile. Mnaona? Kasema, “Lilikuchukua likakupeleka upande wa magharibi. Nami nikalia, na kutembea barabarani.”

²⁷⁷ Kasema, “Baada ya kitambo kidogo nikaondoka nikaenda nikaketi mezani. Nikawa nimeangalia pale upande wa mbele wa ile meza.” Kasema, “Ningeweza kuona tu kiasi *hiki* chako, ulikuwa mweupe kama theluji.” Kasema, “Ulikuwa umesimama

pale.” Kisha kasema, “Ulinena kwa mamlaka. Hakukuweko na kukisia katika jambo hilo.” Kasema, “Kila mtu alifahamu yale hasa uliyokuwa unasema.”

²⁷⁸ Loo, ndugu yangu, dada, sasa, kila mmoja wenu anafahamu moyoni, najua hilo linamaanisha nini. Mnaona?

²⁷⁹ Iweni tu macho! Kaeni karibu na Kristo. Hebu niwaonye sasa, kama mhudumu wa Injili, juu ya jambo hili. Msichukue upumbavu wo wote. Msiwazie cho chote. Kaeni moja kwa moja pale mpaka huu wa ndani wa ndani umetiwa nanga kwenye Neno, mpaka uwe ndani ya Kristo kabisa, kwa maana hicho ndicho kitu pekee ambacho kitaninino... Kwa maana, tuko katika wakati wa udanganyifu sana tuliopata kuishi ndani yake. “Utawapoteza walio Wateule kama yamkini,” kwa maana wana upako, wanaweza kufanya cho chote kama wengine wao.

²⁸⁰ Yasafisheni maisha yenu. Lipeni deni zenu. “Msiwiwe na mtu ye yote,” Yesu alisema. Sasa, sasa, namaanisha, kama kodi yenu ya nyumba na kadhalika, huna budi kufanya hivyo. Ondoa mambo yote mikononi mwako. Weka kila kitu sawa. Iweni tayari. Jitayarisheni. Kumbukeni, katika Jina la Bwana, kitu fulani kiko karibu kutukia.

²⁸¹ Ninaenda milimani juma hili, si hasa kuwinda kindi; naam, napenda kuwinda kindi. Bali naenda kule kwa kusudi hili, nikisema, “Ee Mungu, sijui nienda upande gani, nami sitaki kukosa jambo hili. Nisaidie.”

²⁸² Niombeeni. Mtafanya hivyo? Nitakuwa nikiwaombea. Natumainia, kwa rehema za Mungu, ya kwamba nitakutana na kila mmoja wenu, na tukutane katika nchi bora zaidi kuliko hii hapa.

²⁸³ Nasi tunakuja hapa kwa sababu gani? Tunafanya nini? Tunakuja hapa, kucheza mchezo? Tunakuja hapa, kukutana kama nyumba ya kulala? [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani mara tatu—Mh.] Ni, Kristo hawezi kuja mpaka Kanisa limekuwa sawa kabisa. Yeye anatungojea. Naamini tuko katika wakati wa mwisho.

²⁸⁴ Angalia kule, kule California. Angalia zile ghasia. Angalia hao watu kumi na tisa waliouawa, ubaguzi wa rangi. Je! sikuwaambia, si muda mrefu uliopita hapa, ya kwamba huyo Martini Luther King angewaongoza watu wake kwenye mauaji ya bure? Ni wangapi wanaokumbuka jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Si hao watu weusi; ni hao viongozi wanaowachochea. Si kuchanganyana, ubaguzi, na cho chote wanachotaka kuliita hilo; ni ibilisi. Hiyo ni kweli. Si kwa watu weupe, weusi; hii ni wote hao. Ni ibilisi.

²⁸⁵ Akili za watu na hoja za binadamu zimevunjika. Hakuna matumaini. Haitumainiki. Kitu hicho chote ni kidonda kilichovunda. Akili za mwanadamu; haziwezi kufanya maamuzi.

²⁸⁶ Mimi si mwanasiasa. Mimi si ninino, wala Democrat wala Republican. Vyote ni vichafu. Mimi ni wa Ufalme mmoja, na huo ni Ufalme wa Yesu Kristo. Hiyo tu. Bali ulipataje kuona kundi la vibaraka kama tulio nao kule sasa, kama lile kundi la Watexas tulio nao kule? “Mbona,” wao wanasema, “cho chote wanachotaka watu! Kama wanataka ukomunisti, tutawapa ukomunisti. Wakitaka kuchangamana, tutawapa kuchangamana. Wakitaka ubaguzi, tutawapa cho chote kile.” Je. . . Mwanamume yuko wapi?

²⁸⁷ Ee Mungu! Hiyo ni kama mimbara. Yuko wapi mwanamume, mwanamume ambaye ni mwanamume, ambaye atasimamia kanuni? Wako wapi wanawake ambao husimamia kanuni? Liko wapi kanisa linalosimamia kanuni? Sina wakati hata mdogo kwa ajili ya roho hafifu, ya kushindwa, inayopatana. Mwanamke ni mwanamke, hebu na awe bibi. Kama mwanamume ni mwanamume, hebu na awe mwanamume.

²⁸⁸ Kama yeye ni rais. . . Wako wapi akina John Quincy Adams wetu? Wako wapi akina Abraham Lincoln wetu, watu wenye msimamo? Yuko wapi Patrick Henry wetu, kasema, “Nipe uhuru ama unipe mauti”?

²⁸⁹ Yuko wapi mtu anayesimamia yaliyo kweli? Yuko wapi mtu ambaye haogopi kuzungumza wazi? Haidhuru, ulimwengu wote unampinga, azungumze lililo kweli; na kulitetea na kulifia. Yuko wapi Arnold von Winkelried wetu tena leo? Yuko wapo mtu mwadilifu? Yuko wapi mtu mwenye roho? Wote ni hafifu sana na wamechanganyikiwa sana hata hawajui wanakosimama.

²⁹⁰ Mungu, jalia nisimame na kanuni za Mtu mmoja, kama mhudumu, Neno la Yesu Kristo. “Kwa maana mbingu na nchi zitapita, bali halitashindwa kamwe. Juu ya Mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu; milango ya kuzimu haitalishinda.”

Na tusimame.

Kibarikiwe kifungo
Kitufungiacho mioyo,
Ushirika wetu wa fikara zetu
Ni kama ule wa mbingu.

Sasa shikaneni mikono ninyi kwa ninyi

Tutawanyikapo mbali,
Hiyo yatufadhaisha;
Lakini tungali pamoja rohoni
Hata tutakutanika.

Hata twonane huko juu!
Hata twonane kwake kwema;
Hata twonane huko juu!
Mungu awe nanyi daima.

²⁹¹ Hebu na tuviinamishe vichwa vyetu sasa, wakati Ndugu Neville anapoturuhusu tufumukane, kwa maombi.

²⁹² Rudini usiku wa leo, sasa. Tunatarajia ibada nzuri sana usiku wa leo, hapa Maskanini. Mungu awabariki. Na mniombee; nitawaombea.

²⁹³ Msifikiri ya kwamba mimi ni shupavu wa dini, marafiki. Msifikiri ya kwamba ninajaribu kuwasukumia kitu fulani. Ninawapenda. Nami nina kanuni fulani, hiyo ni Biblia. Hakuna Neno moja linaloweza kuondolewa Kwake. Hakuna Neno moja linaweza kuongezwa Kwake. Nami naliadini namna lilivyoandikwa.

²⁹⁴ Na tuviinamishe vichwa vyetu sasa, kisha mchungaji wetu mwaminifu na mwema aruhusu mkutano ufumukane. Mungu akubariki, Ndugu Neville.



NAWE HUUJI SWA65-0815

(And Knoweth It Not)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili, tarehe 15 Agosti, 1965 katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1992 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org